**Serikali** kumega eneo la Hifadhi ya Taifa iwape wananchi

UKURASA 2



**Upelelezi** kesi ya kuua mke, kumchoma wakamilika

UKURASA 5


Ukurasa 12
Siasa zinavyokoleza migogoro Kigamboni
Ukurasa 13
Rais Dk. Samia akiwekeza kumwinua mama kila kona zinazoamua nchini
siasa
JUMATANO JUNI 28, 2023
Nipashe
HABARI BORA NA KAMILIFU
Ukurasa 14
UASI WA WAGNER
Unavyoleta mkanganyiko vita vya Russia, Ukraine
KATIBA MPYA
Chongolo aamsha mapya, huenda yajayo yakasikitisha, wadau wahofia haitakuwapo
Na Sabato Kasika

UKURASA 11


# Nipashe

Jumatano Juni 28, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

ISSN 0856 • Na. 0581355

nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital epaper.ippmedia.com www.ippmedia.com 0745 700710 LIKE & FOLLOW US


# Mshtuko miamala ya harufu rushwa

• **Ni** yenye thamani ya Sh. trilioni 2/-, taasisi yaipa mbinu serikali kutatua tatizo... *Endelea ukurasa 2*

## Mwema ataja mambo matano kukabili rushwa polisi



UKURASA 3



Wananchi wakichagua mbuzi Vingunguti, Dar es Salaam jana kwa ajili ya maandalizi ya sikukuu ya Eid El-Adha. Mbuzi mmoja aliuzwa kwa bei ya 100,000/- hadi 150,000/- kulingana na ukubwa wake. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Mfanyabiashara aliyedaiwa kujaribu mara mbili kujiua, ajinyonga stoo

UKURASA 3

**MICHEZO** SIMBA YAANIKA HATIMA MKATABA NA SAWADOGO UK.24

**KATUNI** UK.6



Baadhi ya wabunge wakitoka nje ya ukumbi wa Bunge jijini Dodoma jana, baada ya kusikika kwa sauti ya king'ora ambapo Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, aliahirisha shughuli kwa muda. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mshtuko miamala yenye harufu ya rushwa nchini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TAASISI ya WAJIBU imezindua ripoti nne za uwajibikaji kwa mwaka 2021/22 huku ikionyesha mashirika ya umma yamekuwa na ongezeko la asilimia 43 ya miamala ambayo ina viashiria vya rushwa, ubadhirifu na udanganyifu.

Kutokana na hali hiyo, taasisi hiyo iliyo chini ya Mkurugenzi Mtendaji Ludovick Utouh, aliyewahi kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), imependekeza serikali kupeleka muswada bungeni wa kuanzisha Sheria ya Ubadhirifu na Udanganyifu (Fraud Act) ili kudhibiti vitendo vya rushwa.

Akiwasilisha dondoo za ripoti hizo jana jijini hapa, Meneja Miradi wa taasisi hiyo, Moses Kimaro, alisema ripoti hizo zimetokana na uchambuzi ripoti za CAG kwa mwaka huo.

Alisema ongezeko la viashiria hivyo ambavyo havijathibitishwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) ni kutoka Sh. trilioni 1.4 kwa mwaka wa fedha 2020/21 hadi Sh. trilioni 2.01 mwaka wa fedha 2021/22.

Meneja huyo pia alipendekeza taasisi za dini ziendelee kuikemea rushwa kwa bidii zote na taarifa ya TAKUKURU inayowasilishwa kwa Rais, iwe inapelekwa bungeni kujadiliwa ili iwe wazi kwa umma na itasaidia kuongeza kasi ya mapambano dhidi ya rushwa nchini.

"Bunge lifanye marekebisho ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kwa kuifanya ripoti yake ya utendaji ya mwaka ya TAKUKURU kuwa wazi kwa umma. Hii itaboresha na kuongeza morali kwa wananchi kuripoti vitendo vya rushwa,"alisema.

Kuhusu usimamizi wa matumizi, meneja huyo alisema pamoja na kuongezeka kwa makusanyo kwa mwaka 2021/22, bado kumekuwa na upungufu katika usimamizi wa matumizi.

Alitaja upungufu uliojitokeza unajumuisha upotevu wa mapato (Sh. trilioni 1.49), ununuzi wa umma na usimamizi wa mikataba (Sh. trilioni 1.17) na matumizi yasiyokuwa na tija (Sh. bilioni 411.3).

Kimaro alishauri nguvu zielekezwe kuboresha mifumo ya ndani pamoja na kuimarisha mifumo ya kidigitali ya usimamizi wa matumizi.

Kuhusu mashirika 45 yaliyobainishwa na CAG kujiendesha kwa hasara, meneja huyo taasisi yao inatoa ushauri kwa Msajili wa Hazina ayafanye mapitio ya utendaji wa mashirika hayo ili kupata suluhu ya namna bora ya kuyaendesha.

"Pia Msajili wa Hazina aangalie mashirika hayo ili kuona kama kuna thamani ya fedha kutokana na mchango wake katika uchumi kulinganisha na hasara yaliyopata,"alisema.

Akizindua ripoti hizo, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Jenifa Omolo, alisema ripoti hizo zitasaidia kuongeza uwajibikaji na uwazi kwa umma ili kujiepusha na vitendo vya rushwa.

"Taifa letu limepiga hatua kubwa katika kupambana na rushwa ingawa bado tunahitaji kuendelea na mapambano hayo, ndio maana siku hizi ninafurahia TAKUKURU wamekwenda kwenye elimu zaidi.

"Serikali imeona umuhimu wa kufanya marekebisho ya Sheria ya Ununuzi wa Umma kutokana na kilio cha muda mrefu,"alisema.

Naibu Waziri huyo alisema serikali inaendelea kufanyia kazi ripoti ya CAG na suala hilo limepewa kipaumbele ili kuboresha utendaji kazi na kuleta tija.

Awali, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Taasisi ya WAJIBU, Yona Killagane, alisema kuwa kwa kushirikiana na wadau wengine, wanajitahidi kuwafikia wananchi wengi ili waelewe dhana ya uwajibikaji.

Alitaja ripoti hizo nne za uwajibikaji ni pamoja na ya usimamizi mapato na matumizi, viashiria vya rushwa, ubadhirifu na udanganyifu katika taasisi za umma, vyombo vya usimamizi na utoaji wa huduma kwa jamii.

Mbali na kuchambua ripoti za CAG, Taasisi ya WAJIBU imekuwa inatoa elimu kwa umma na waandishi wa habari kuhusu dhana ya uwajibikaji, na hata kuwawezesha kifedha waandishi wa habari kwenda katika maeneo yenye shida kiuwajibikaji na kuibua udhaifu.

## Wabunge waridhia kuongeza mipaka Hifadhi ya Taifa Ruaha

**Na Jenifer Gilla,** DODOMA

BUNGE jana lilipitisha Azimio la Bunge kuridhia pendekezo la kufutwa hadhi ya Hifadhi ya Kigosi ili kuruhusu kuanzishwa Msitu wa Hifadhi ya Kigosi na kurekebisha mipaka ya Hifadhi ya Taifa Ruaha (RUNAPA), kuruhusu ushirikishwaji wa wananchi katika shughuli za kiuchumi.

Akiwasilisha maazimio hayo, Waziri wa Maliasili na Utalii, Mohamed Mchengerwa, alisema mabadiliko hayo yatatoa fursa na manufaa ya kimazingira na kiuchumi kwa wananchi wanaoishi maeneo yanayozunguka hifadhi hizo.

Alisema lengo la serikali la kufuta Hifadhi ya Kigosi ni kuruhusu kuanzishwa kwa Hifadhi ya Msitu Kigosi ambao utasimamiwa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) chini ya Sheria ya Misitu Sura 323, kwa ajili ya wananchi kufanya shughuli mbalimbali za kiuchumi.

Mchengerwa alisema msitu huo utatoa fursa kwa ufugaji, kurina asali na uwindaji kwenye mikoa ya Geita, Kagera, Kigoma, Shinyanga na Tabora kwa wilaya sita na vijiji 125 hali itakayowainua kiuchumi.

"Kutachochea shughuli za kibiashara ikiwamo ufugaji nyuki kibiashara ili takriban wafugaji 1,764 wenye mizinga zaidi ya 521,406 waliokuwapo awali kwenye maeneo hayo wataongezeka maradufu," alisema.

Vilevile, hatua hiyo itachangia ongezeko la uzalishaji wa asali nchini kutoka wastani wa tani 32,691 hadi 138,000 kwa mwaka na kuongeza mauzo ya mazao ya nyuki nje ya nchi na kuongeza mchango wa sekta ya misitu na nyuki katika Pato la Taifa.

Kuhusu azimio la marekebisho ya mipaka ya RUNAPA, Mchengerwa alisema yanalenga kutatua migogoro ya mipaka baina ya hifadhi na vijiji uliokuwapo tangu 2018, baada ya wanakijiji kulalamika kutoshirikishwa katika uwekaji wa vigingi vya mipaka.

Marekebisho hayo pia yatasababisha kupatikana kwa eneo lenye ukubwa wa kilometa za mraba 478 ambalo litamegwa kutoka sehemu ya hifadhi kwenda katika vijiji 29 kwa ajili ya shughuli mbalimbali za kiuchumi ikiwamo kilimo na ufugaji.

Litachangia kuhifadhi vyanzo vya maji katika Bonde la Usangu na kuimarisha mtiririko wa maji kwenye milima ya Kipengere na Uporoto kuelekea lindimaji la Ihefu ambalo ni chanzo cha Mto Ruaha Mkuu unaotegemewa kuzalisha umeme wa maji katika mabwawa ya Mtera, Kidatu na Bwawa la Julius Nyerere ili kuimarisha upatikanaji wa umeme nchini.

### MAONI YA KAMATI

Akisoma maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, kuhusu azimio la kuruhusu kuanzishwa kwa Hifadhi ya Msitu ya Kigozi, Makamu Mwenyekiti wa kamati, Najma Giga, alisema kamati inaushari serikali pamoja na mambo mengine kuelimisha wananchi walio karibu na msitu huo.

Pia wananchi hao pamoja na wawakilishi wao washirikishwe kikamilifu katika michakato ya kubadili mipaka au matumizi ya maeneo ili wawe na uelewa wa pamoja kuhusu dhamira ya serikali na mantiki ya michakato hiyo.

Kamati hiyo imesisitiza kusiwe na jambo lolote litakalozuia serikali kuchukua hatua stahiki kwa manufaa ya taifa, hata kama kufanya hivyo kutakuwa na gharama kubwa ili kulinda hifadhi kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Kuhusu marekebisho ya mpaka katika RUNAPA, Mwenyekiti wa kamati, Timotheo Mnzava, alisema kamati imependekeza serikali ihakikishe zoezi la kuhakiki na kuweka alama za mpaka linawashirikisha wananchi na wawakilishi wao.

Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Neema Mgaya, alisema kurekebisha mpaka wa RUNAPA kutasaidia kutatua migogoro mbalimbali kati ya wananchi na hifadhi, ikiwamo mgogoro wa Mbarali uliokuwapo tangu mwaka 2018.

Mbunge wa Jimbo la Ushetu (CCM), Emanuel Cherehani, aliishauri serikali kuhakikisha kuwa inawasajili wafugaji, warina asali, wavuvi na wachimbaji wadogo watakaofanya shughuli za uzalishaji katika Hifadhi ya Kigosi, ili watambulike na kunufaika na rasilimali inayopatika na msitu huo.

HABARI KITAIFA

# Mwema atoa mbinu kuikabili rushwa Polisi

**Na Halfani Chusi**

MKUU wa Jeshi la Polisi mstaafu, Said Mwema, amependekeza mbinu za kukabiliana na rushwa ndani ya jeshi hilo.

Katika kitabu chake chenye sura tisa alichokipa jina la 'Polisi Utawala na Usimamizi wa Sheria Tanzania Mkakati Kubadilisha Mwelekeo', Mwema ameitaja mikakati mitano inayopaswa kutumia na jeshi hilo kupambana na rushwa.

Kiongozi huyo ambaye mbali na kulitumikia Jeshi la Polisi, ana taaluma ya sheria, pia ameainisha mbinu za kuboresha mfumo wa utawala ndani ya jeshi hilo, ili kufikia lengo la kuwa na jeshi linalozingatia utii wa sheria, weledi na haki za binadamu.

Kwa mujibu wa Mwema, mikakati ya kupambana na rushwa ndani ya Jeshi la Polisi inajumuisha kuchukua hatua kali dhidi ya wala rushwa wote kwa kuanzisha hatua za kuzuia ikiwamo kutambua aina ya mianya ya rushwa ndani ya utendaji na kuiziba.

Katika kitabu hicho ambacho dibaji yake imeandikwa na Rais wa Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete, Mwema anataja mbinu nyingine ni kuchukua hatua za makusudi, zilizoainishwa katika kuzuia vitendo hivyo ndani ya polisi kama zilivyo kwenye sheria, kanuni na amri za jeshi.

Pia anapendekeza kuchukuliwa hatua za makusudi katika kuzuia vitendo vya rushwa ndani ya polisi; kusimamia uwazi, uadilifu na uwajibikaji katika utoaji wa huduma za polisi; na kuziwezesha kamati za maadili pamoja na mikakati, utendaji na mbinu za kiongozi, kusimamia maadili katika maeneo yao.

**JESHI LA KISASA**

Mwema pia ana mapendekezo saba yanayopaswa kufanyiwa kazi ili kuifikia ndoto ya kuwa jeshi la kisasa.

Anayataja katika kitabu hicho yanajumuisha kuhakikisha uratibu bora wa mageuzi unafanyika, kukuza mabadiliko ya mitazamo inayounga mkono mageuzi, kutengeneza sera kuu ya usalama wa taifa na mifumo ya kisheria.

Pia nasema kuna haja kuendeleza na kukuza uwezo wa uchambuzi katika masuala na mifumo ya uwajibikaji na ya kiutendaji, kuwezesha kujenga uwezo katika ngazi ya juu na chini ya serikali za mitaa na kutengeneza mkakati na mpango wa kina wa ushiriki wa wadau.

Kitabu hicho kilizinduliwa mwishoni mwa wiki iliyopita jijini Dar es Salaam na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Jumanne Sagini.



Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (DAWASA), Kiula Kingu (mwenye fimbo), akitoa maelezo kwa Balozi wa China nchini, Chen Mingjian (wa pili kulia), kuhusu utekelezaji wa awamu ya tatu ya mradi wa maji Chalinze kwa eneo la upanuzi wa mtambo wa kuzalisha maji wa Wami alipotembelea jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

## Raia China kortini tuhuma kukutwa na jongoo bahari

**Na Grace Gurisha**

RAIA wa China, Wei Zhang (54) amepandishwa kizimbani Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam kwa tuhuma za kukutwa na jongoo bahari kilo 4.10.

Zhang alifikishwa mahakamani hapo jana na kusomewa shtaka linalomkabili na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Grace Mwanga mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shahidi, aliyedai mshtakiwa anatuhumiwa kwa shtaka moja.

Alidai kuwa Zhang alitenda kosa hilo Aprili 7, mwaka huu akiwa eneo la Mtaa wa Kumbukumbu wilayani Kinondoni jijini Dar es Salaam.

Imedaiwa siku hiyo, Zhang alikutwa akiwa na kilo 4.10 za jongoo bahari (sea cucumber) huku akijua kuwa jamii hiyo ya jongoo bahari ipo hatarini kutoweka na ni kinyume cha sheria.

Hata hivyo, Zhang alikana kuhusika na tuhuma hizo, upelelezi wa kesi hiyo umekamilika.

Hakimu Shaidi alisema dhamana ipo wazi kwa mshtakiwa, anatakiwa awe na wadhamini wawili wakazi wa Dar es Salaam.

Wanatakiwa kuwa na vitambulisho vya taifa pamoja na barua ya utambulisho kutoka serikali za mitaa na kusaini bondi ya Shilingi milioni tano.

Kesi hiyo imeahirishwa hadi Julai 5, mwaka huu itakaporudi tena mahakamani hapo kwa ajili ya mshtakiwa kusomewa hoja za awali.

## Mfanyabiashara ajiua kwa kujinyonga stoo

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

MFANYABIASHARA maarufu wa maduka ya vyakula jijini Tanga, Hamisi Rashid (53), amejinyonga kwa waya hadi kufa baada ya kujifungia kwenye stoo yake ya kuhifadhi bidhaa.

Kabla ya tukio hilo, imedaiwa aliwahi kujaribu kujiua mara mbili mfululizo kwa kutumia kamba ngumu ya katani ikiwa juu ya kitanzi cha mbao na kukatika.

Kamanda wa Polisi, Mkoa wa Tanga, Kamishna Msaidizi (ACP), Henry Mwaibambe, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo usiku wa Juni 27, mwaka huu.

"Taarifa kuhusu tukio hili, tumeipokea kutoka kwa mke wa marehemu, Mwanaidi Issa, kuwa mumewe alijinyonga akiwa nyumbani kwake, Kata ya Makorora.

"Lakini sababu za yeye (Hamisi) kujitoa uhai, bado hazijajulikana. Tumeanza kuchunguza kifo hicho," alisema Kamanda Mwaibambe.

Katika tukio jingine, watu wasiojulikana wamemuua kwa kumpiga na kitu chenye ncha kali kichwani, mwendesha pikipiki (bodaboda), Damian Pius (24), mkazi wa kitongoji cha Kongwa-Amboni, Kata ya Mzizima.

Damian, alikutwa amefariki dunia jana katika Barabara Kuu ya Horohoro/Tanga, eneo la daraja la Utofu, akiwa na jeraha kichwani.

"Katika tukio hili, tumemkamata mtuhumiwa mmoja Oscar Haule (26), ambaye ni bodaboda, kwa ajili ya uchunguzi.

"Kwa mujibu wa watoa taarifa wetu, eneo la tukio walikuwapo bodaboda watatu, baada ya mwenzao kuanguka. Walianza kugombania mirungi (dawa za kulevya) ambazo zilikuwa zimehifadhiwa katikati ya gunia la mkaa," alisema Kamanda Mwaibambe.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
26 . 06 . 2023

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Ndugu Wananchi mnatangaziwa kua siku ya tarehe **27.06.2023** hadi **10.07.2023** kampuni ya **CEVA Interfreight** itasafirisha gari tupu wenye vipimo vikubwa kutoka Mzenga kuelekea Bandari ya Dar Es Salaam, gari hilo lenye namba za usajili

**NRB97300 / NRB54202**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:

**Urefu - mita 29.00 Upana - mita 4.30 Kimo - mita 4.60**

3. Njia itakayotumika: **Mzenga** hadi **Bandari ya Dar Es Salaam** kupitia **Barabara ya Morogoro, Barabara ya Mandela** gari litasafiri muda wa mchana ( **Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni).**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza**

# The Guardian Limited yachangia kampeni ya EATV 'Namthamini'

**Na Mary Kadoke**

KAMPUNI ya The Guardian Limited imechangia katoni 50 za taulo za kike kwa ajili ya kuunga mkono msimu wa saba wa kampeni ya 'Namthamini' inayoendeshwa na Kituo cha Televisheni cha East Africa (EATV) na Kituo cha Redio cha East Africa (EARadio) inayolenga kuwasaidia wanafunzi wa kike.

Mchango huo ulikabidhiwa jana makao makuu ya EATV Mikocheni, jijini Dar es Salaam na Mhariri Mtendaji wa Gazeti la Nipashe, Beatrice Bandawe.

Kampeni hiyo inalenga kunufaisha wanafunzi wa kike 10,000 katika mikoa minne ambayo ni Katavi, Mara, Geita na Kilimanjaro.

Mhariri Mtendaji wa gazeti la Nipashe, Bandawe, alisema msaada huo umelenga kusaidia wanafunzi wa kike wanaokatisha masomo yao kipindi cha hedhi kwa kukosa vifaa salama vya kujihifadhi.

"Kampuni ya The Guardian imechangia katoni 50 za taulo za kike kwa ajili ya ku- 'sapport' kampuni dada katika kampeni yao ya 'Namthamini' ili kuwasaidia wanafunzi wa kike wanaoshindwa kuendelea na masomo yao kila mwezi kwasababu ya kukosa vifaa kwa ajili ya kujihifadhi," alisema.

Aliongeza: "Kama kampuni dada tunaalika wadau wengine kuunga mkono kampeni hiyo, ili kusaidia wasichana wanaotarajiwa kuwa viongozi wa baadaye, wasikatishe ndoto zao kwa kukosa masomi wanapokuwa kwenye siku zao za hedhi."

Balozi wa Namthamini wa EATV, Justine Kessy, alipongeza hatua iliyochukuliwa na Kampuni ya TGL, ambayo kwa asilimia kubwa imenufaisha wanafunzi wa kike kupitia kampeni hiyo.

"Tunaipongeza The Guardian Limited kwa kuunga mkono kampeni yetu katika kila msimu wa kampeni ya 'Namthamini'. Tumeamua kuendesha kampeni hii kwa kufungua pia milango kwa wadau wengine, ili kusaidia wasichana wanaotarajiwa kuwa viongozi wa baadaye," alisema.

Kampeni hii ilianza mwaka 2017 baadaye kupokea ripoti kwamba wanafunzi kati ya 50 mpaka 60 wanakatisha masomo yao kila mwaka kwa kukosa taulo za kujihifadhi.

Kampeni hii imenufaisha mikoa 19 mpaka sasa ikiwamo Arusha, Kagera, Dar es Salaam, Lindi, Coast, Tabora, Tanga na Singida. Hata hivyo wilaya 80 zimenufaika na kampeni hiyo mpaka sasa.



Mhariri Mtendaji wa Gazeti la Nipashe, Beatrice Bandawe (kushoto), akikabidhi taulo za kike katoni 50 kwa Balozi wa kampeni ya Namthamini inayoendeshwa na East Africa Radio na EATV, Justine Kessy zilizotolewa na Kampuni ya The Guardian Ltd inayochapisha magazeti ya The Guardian na Nipashe, Mikocheni, Dar es Salaam jana, kwa ajili ya kusaidia wasichana wanafunzi. **PICHA: JOHN BADI**

## Kizimbani tuhuma kunajisi mtoto wa umri miaka 14

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MKAZI wa Kijiji cha Izumacheli, Fadhili Elisha (19), amefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Geita kwa kosa la kumnajisi msichana mwenye umri wa miaka 14 ambaye ni mwanafunzi wa Shule ya Msingi Izumacheli.

Mshtakiwa huyo amepandishwa kizimbani jana mbele ya Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Nyakato Bigirwa na aliposomewa mashtaka, alikana kuhusika na kosa hilo na yuko mahabusu katika Gereza la Wilaya ya Geita kutokana na kukosa wadhamini.

Upande wa Mashtaka ukiwa na Mawakili wawili wa Serikali Godfrey Odupoy na Kabula Benjamini, ulidai upelelezi wa kesi hiyo umekamilika na kuomba tarehe nyingine kwa ajili ya kumsomea mshtakiwa huyo maelezo ya awali.

Hakimu Bigirwa alikubaliana na ombi hilo na kuahirisha kesi hiyo hado Julai 10 mwaka huu kwa ajili ya kumsomea mshtakiwa maelezo ya awali.

Hakimu Bigirwa aliyataja masharti ya dhamana kwa mshtakiwa huyo ni kuwa na mdhamini mmoja mwenye barua ya utambulisho kutoka kwa Ofisa Mtendaji wa Kata na mali isiyohamishika yenye thamani ya Sh. milioni mbili.

Akisoma hati ya mashtaka jana, Wakili wa Serikali, Godfrey Odupoy, alidai kuwa katia tarehe tofauti mwaka 2023, kijijini Izumacheli, Mkoa wa Geita, mshtakiwa alimnajisi msichana mwenye umri wa miaka 14 ambaye ni mwanafunzi wa Shule ya Msingi Izumacheli na kumsababishia maumivu makali sehemu zake za siri.

# Kanzidata taarifa za kifua kikuu SADC yazinduliwa

**Na Salome Kitomari**

SHIRIKA la East Central and Southern Africa Health Community (ECSA-HC) limezindua kanzidata ya kuhifadhi takwimu za mwenendo wa ugonjwa wa kifua kikuu (TB) katika migodi ndani ya nchi 16 za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), ambazo zimeathiriwa kwa kiasi kikubwa.

Kanzi data hiyo imeandaliwa na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), na imezinduliwa rasmi jana wakati wa mkutano wa nchi wanachama 16, kujifunza inavyofanya kazi kwa ajili ya kuanza kuitumia na kuwezesha taarifa kuonekana kwa urahisi zaidi na kusaidia kwenye maamuzi ya kisera kwa maendeleo ya nchi husika.

Uzinduzi huo umefanyika wakati ECSA-HC inaendelea na utekelezaji wa awamu ya tatu ya mradi wa Kudhibiti Tishio la Kusambaa TB katika Migodi (TIMS) kwenye nchi wanachama ili kuwafikia waathirika na kuwaepusha maambukizi mapya.

"Waliokutana hapa ni mamenenja, wafanya ufuatiliaji na tathmini pamoja na maofisa progaramu wanaokutana kuanza kutumia kanzi data ambayo ni muhimu kuwezesha upatikanaji wa taarifa. Tuna mradi mkubwa ambao awali ulikuwa kwenye nchi 10 na sasa tumeongeza hadi 16," alisema Mkuu wa Kitengo cha Afya na Lishe wa SADC Secretariat, Dk. Willy Amisi.

Alisema Tanzania ni moja ya nchi tisa inayojulikana kwa kuwa na maambukizi makubwa ya kifua kikuu migodini na ndiyo sababu ya mkutano huo kufanyika nchini ili kuwa na kanzi data itakayowezesha kila mmoja kuona taarifa za nchi nyingine tofauti na utaratibu wa awali kila mmoja alizikusanya na kuwa nazo kwenye ofisi.

"Data hizi zitasaidia katika utengenezaji wa sera za ukanda wa SADC kwa urahisi zaidi tofauti na awali ililazimu kufutafuta viongozi wa nchi husika, hii ni hatua kubwa sana kwa nchi zetu. Nashauri nchi wanachama kuongeza kasi ya kuingiza data kwenye mfumo, tuunganishe nguvu katika kukabili TB," alisema Dk. Amisi.

Naye Mkurugenzi wa Operesheni na Maendeleo ya Taasisi wa ECSA-HC, Sibusisa Sibandze, alisema mradi huo utawagusa wananchi wa kawaida kwa kuwa moja ya eneo la utekelezaji ni usimamizi wa haki za wachimbaji wadogo na familia zao, ikiwamo kupata vifaa na tiba sahihi na kwamba maisha yao yaendelee hata wanapoondoka kwenye sekta ya madini.

"Katika awamu ya kwanza ya mradi hatua kubwa zimechukuliwa ikiwamo kulinda haki za wachimbaji wadogo na familia, tumekuja na sera jumuishi kwenye haki za binadamu na wanawake wanaofanyakazi migodini, kwa awamu hii ya pili tutahikisha kila jambo limeelezewa kwa kina, tutawafikia wachimbaji wote kwenye nchi zote 16," alisema Sibandze.

Alisema kanzi data hiyo ni muhimu sana kwa nchi na SADC kwa kuwa zitasaidia kuona hali halisi kwenye nchi na kama kuna matokeo chanya au la na kwamba ambako panahitaji nguvu zitaelekezwa huko kuhakikisha malengo yanafikiwa.

Alisema nchi zote zimejitahidi kuwa na Mpango wa Taifa wa Kifua Kikuu, Mpango mkakati, Sera za TB na sera ya SADC kwa ajili ya TB, ambazo zinatekelezwa na kwamba kwa mradi huo itaongeza kasi kwenye maeneo mengi ikiwamo kuwa na bajeti maalumu kwa ajili ya TB licha ya changamoto za kifedha.

Mchambuzi wa mifumo kutoka UDSM ambao ndiyo watengenezaji wa mfumo huo, Merina Luambano, alisema kanzi data hiyo ni moja ya kazi waliyofanya ya kuboresha mifumo ya taarifa kwenye sekta ya afya na kwamba itasaidia kuongeza upatikanaji wa data na kuiwezesha nchi kufanya maamuzi.

"Kwa kutumia mfumo zitaripotiwa na kuchakatwa kwa wakati tofauti na utaratibu wa awali wa kawaida, nchi 16 zitaweka taarifa zake. Tulianza mwaka 2022 na tumeshakamilisha na tunaukabidhi wa SADC kwa ajili ya kuutumia na wataweza kuingiza taarifa za nyuma ambazo walizitunza kwa njia nyingine," alisema.

Kwa mujibu wa Ripoti ya Shirika la Afya Duniani (WHO), ya mwaka jana, mataifa 30 yapo katika kiwango cha juu cha maambukizi ya ugonjwa wa TB huku Tanzania ikiwa ni kati ya nchi nane za SADC zenye tishio kubwa la maambukizi migodini.

# RAS apata mwarobaini ukosefu wa dawa vituoni

**Na Mary Geofrey**

KATIBU Tawala Mkoa wa Dar Salaam amewataka watoa huduma za afya kuhakikisha wanawasilisha maombi ya dawa na vifaa tiba mapema katika Bohari ya Dawa (MSD) ili kupatiwa dawa kwa wakati na kuondokana na tatizo la wananchi kukosa huduma.

Rehema Madenge alitoa rai hiyo jana jijini Dar es Salaam alipozungumza na wadau wa huduma za afya kwa lengo la kujadili njia za kuhakikisha huduma zinapatikana kwa wakati.

Mkutano huo uliandaliwa na MSD Kanda ya Dar es Salaam, inayounganisha mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro na Zanzibar.

Alisema amefanya ziara na kubaini ghala la hifadhia dawa MSD limesheheni dawa zinazotakiwa kufikia kwa wahitaji haraka lakini changamoto inatokana na ucheleweshwaji wa maombi ya kupata huduma.

"Nitoe wito na kusisitiza katika hili, tunalo jukumu la kufanya sisi watoa huduma na MSD kuhakikisha tunapeleka maombi mapema na kwa wakati ili kupata huduma haraka kabla hujamaliza dawa ulizonazo stoo," alisema.

Alisema njia hiyo itasaidia kuongeza thamani ya fedha na kusaidia upatikanaji wa huduma kwa wakati badala ya kuendelea kubakia na tatizo la upatikanaji huduma kwa wakati.

Katibu Tawala pia alisisitiza usimamiaji wa makusanyo ya fedha za huduma za bidhaa za afya ili kusaidia kupata huduma kwa haraka na kwa wakati.

Awali, Mganga Mkuu wa Dar es Salaam, Rashid Mfaume, alihimiza ushirikishwaji kutoka kwa watoa huduma za afya kwenda MSD na namna wanavyoweza kutatua vikwazo vya upatikanaji wa huduma kwa wakati.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa MSD, Leopold Shayo, aliahidi kuendelea kutoa huduma zilizotukuka kwa wadau wa afya kama ambavyo imeendelea kuongeza kasi ya uzalishaji wa huduma hiyo.

Alisema wanaendelea kuboresha huduma kila mara na kukutana na wadau wanaofanya nao kazi ili kusawazisha kasoro zinazojitokeza ili kuhakikisha Watanzania wanapata huduma.

Awali, Meneja wa MSD Kanda ya Dar es Salaam, Betie Kaema, alisema wamekutana na wataalamu wa dawa na wafamasia kanda hiyo, kwa lengo la kubadilisha mawazo, kupeana mikakati na mrejesho wa namna wanavyopata huduma zao.

"Tumefanya kazi kubwa ya kuhakikisha tunakidhi uhitaji wa bidhaa za afya kwa Watanzania wote, tunazalisha vifaa tiba vya kutosha na dawa lakini kuzisambaza maeneo yote," alisema.

# Upelelezi wakamilika kesi ya kuua mke, kumchoma

**Na Grace Gurisha**

MFANYABIASHARA Khamis Luwonga (38) anayetuhumiwa kumuua mkewe, Naomi Marijani na kumchoma moto kwa kutumia magunia mawili ya mkaa, anatarajiwa kusomewa maelezo ya mashahidi na vielelezo vitakavyotumika katika kesi keshokutwa baada ya upelelezi kukamilika.

Luwonga alitakiwa kusomewa maelezo hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Ramadhani Rugemalira wa Mahakama ya Hakimu Mkazi, Kisutu, Dar es Salaam, lakini ilishindikana kutokana na hati ya wito kuchelewa kupelekwa kwa mshtakiwa gerezani.

Kutokana na hali hiyo, mahakama iliahirisha mshtakiwa huyo kusomewa 'committal' hadi Ijumaa saa mbili asubuhi kwa kuwa Luwonga hakuwapo mahakamani.

Awali, Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam ilisema kulingana na sheria inavyotaka haina mamlaka ya kufanya uamuzi wa kumwachia huru mshtakiwa kama mawakili wake walivyoomba kwa madai kuwa yupo gerezani kimakosa.

Mahakama hiyo pia ilielekeza kwamba jalada la kesi hiyo lirudishwe katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu ili hakimu anayeisikiliza shauri hilo atolee uamuzi juu ya uhalali wa kuwapo kesi hiyo ya mauaji katika mahakama hiyo.

Uamuzi huo ulitolewa na Jaji Obadia Bwegoge baada ya mshtakiwa kupitia mawakili wake, Mohamed Majaliwa, Fatuma Abdul na Zidadi Mikidadi kuwasilisha mahakamani hapo maombi ya kutaka kupata maelezo ya uhalali wa kesi hiyo ya mauaji.

Katika kesi ya mwaka 2019, mshtakiwa Luwonga ambaye ni Mkazi wa Kigamboni, Dar es Salaam, anadaiwa Mei 15, 2019 akiwa Gezaulole, Kigamboni, alimuua Naomi.

Inadaiwa kuwa mshtakiwa huyo alimuua mke wake huyo kisha kumchoma moto kwa kutumia magunia mawili ya mkaa na baadaye kuchukua majivu ya mwili wa marehemu na kuyafukia shambani kwake.




Kamishna wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), Dk. Baghayo Saqware (kulia), akiwa na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Strategis, Dk. Flora Minja (katikati) na Ofisa Mtendaji Mkuu-Bima za Mali na Majanga, Jabir Kigoda, wakipiga makofi kuashiria uzinduzi rasmi wa Bima ya Kilimo ya Strategis Insurance jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wabunge wacharuka Mchuchuma, Liganga

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MRADI wa Mchuchuma na Liganga umewaibua wabunge, wakitaka majibu sahihi ya serikali kutokana na kujadiliwa kwa muda mrefu bila kufikia tamati.

Jana katika kipindi cha Maswali bungeni, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Neema Mgaya, ahoji lini serikali itakamilisha mkataba wa mwekezaji ili mradi wa Liganga na Mchuchuma ufanye kazi na kuchangia Pato la Taifa na kukuza uchumi.

Mbunge huyo pia alihoji muda ambao itatolewa fidia za mradi wa makaa ya Maganga Matitu na Katewaka wilayani Ludewa na lini majadiliano na mwekezaji yataisha ili mkataba utiwe saini na mradi uanze kufanya kazi.

Mbunge wa Kinondoni (CCM), Tarimba Abbas, alihoji utayari wa serikali kutekeleza mpango kazi utakaoonyesha muda wa kutekelezwa mradi huo badala kusema majadiliano yanaendelea.

Mbunge wa Simanjiro (CCM), Christopher Ole Sendeka, alisema mradi huo awali ulikuwa unaipa Tanzania asilimia 20 na asilimia 80 inakwenda kwa mwekezaji ambaye uwekezaji wake ulikuwa wa Dola za Marekani milioni 600 badala ya Dola za Marekani bilioni tatu zilizokuwa zinahitajika.

Mbunge wa Bunda (CCM), Boniphace Getere, alisema inadaiwa mwekezaji wa awali ana tatizo na serikali na uwezo wake ni mdogo.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe, alisema serikali imeanza upya majadiliano na mwekezaji wa mradi huo ili kuhakikisha haululeti hasara kwa taifa.

Naibu Waziri Kigahe alisema serikali imedhamiria kuona mradi unganishi wa Liganga na Mchuchuma unatekelezwa na kwa kuzingatia dhamira hiyo hatua mbalimbali zimeanza kuchukuliwa ili kuanza utekelezaji wa mradi huo muhimu.

"Hatua hizi ni pamoja na kulipa fidia ya Sh. bilioni 15.42 kwa wananchi 1,142, pia tumeanza upya majadiliano na mwekezaji wa mradi ili kuhakikisha mradi utatekelezwa pasi na kuleta hasara kwa Taifa," alisema Kigahe.

Alisema serikali inatambua umuhimu wa mradi huo na hatua nzuri zimefikiwa na majadiliano yatakamilika mapema ili kuanza utekelezaji wa mradi bila vikwazo.

Kigahe alisema kupitia diplomasia ya uchumi wamefikia hatua nzuri kukamilisha majadiliano na wawekezaji hao ambao awali walikuwa hawafiki katika majadiliano na kwamba majadiliano hayo yanaendelea bila vikwazo au vivutio walivyotaka ambavyo vilikuwa ni hasara kwa taifa.

Alimhakikishia mbunge huyo kuwa mradi huo ukimalizika, wataanza utekelezaji wa miradi mingine ya Maganga Matitu na Katewaka.

Kuhusu uwezo wa mwekezaji, alisema wamefanya ufuatiliaji na moja ya vitu vilivyoonekana alikuwa na uwezo mdogo na katika majadiliano ya hivi karibuni amesema ana uwezo wa kufanya na serikali inaendelea kuangalia kama kuna mwekezaji mwingine ambaye ataweza baada ya kumalizana na huyo wa awali iwapo atashindwa.

Kutokana na majibu hayo, Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, aliitaka serikali kujipa muda huku akihoji majadiliano hayo yataisha lini.

"Kama mkishindwa, tafuteni mwekezaji mwingine sio lazima mkae naye miaka na miaka kwa sababu upungufu wa hapo hili jambo litakuwa linarudi na kurudi na mkiendelea kumshikilia huyo huyo tunakuwa hatuelewi kidogo," alisema.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Mashimo barabarani ni kero inayohitaji suluhisho la kudumu

**BAADHI** ya barabara katika Jiji la Dar es Salaam, haziko katika hali ya kuridhisha kutokana na mashimo yaliyoibuka baada ya mvua ya masika iliyonyesha kwa takribani miezi mitatu.

Mashimo hayo yamejaa kwenye baadhi ya barabara na kusababisha usumbufu kwa magari ambayo mengine huyaingia kwa bahati mbaya na kufanya uharibifu.

Mbali na kusababisha uharibifu, mashimo yamekuwa kero kwa kusababisha foleni wakati madereva wakijaribu kuyakwepa.

Hili tatizo la mashimo barabarani ni hatari kwa sababu wakati mwingine husababisha ajali madereva wanapoyakwepa uhama kwenye upande wanaostahili kuwapo na kwenda upande mwingine.

Watumiaji wa barabara wanahoji inakuwaje mashimo hayo yanapotengenezwa hayachukui muda mrefu yanachimbika tena. Wakati mwingine hata mwezi mmoja hautimii.

Je, wanaopewa kufanya kazi ya kuziba mashimo hayo wanafanya kwa kuzingatia viwango au wanalipua ili yaharibike haraka wapate kazi nyingine tena ya kuziba mashimo hayo.

Kwa baadhi ya barabara hasa ile inayoanzia kwenye makutano ya ofisi za kampuni ya simu ya Zantel inayokwenda mpaka kwenye mataa ya Africana, imeshamiri kwa viraka na mashimo na kuwa kero kubwa kipindi cha asubuhi watu wanapokwenda kwenye shughuli zao za kazi na jioni wanaporudi majumbani mwao.

Kitu kingine kinachokera, mafundi wanaokarabati barabara hizo wanapokata sehemu zilizochimbika, wanaziacha kwa muda mrefu bila kuziba sehemu hizo walizozikata na kuzichimba.

Kama wanaamua kufanya ukarabati ni vyema wakasubiri mpaka bajeti waliyopangiwa ikamilike na kuifanya kazi hiyo kwa wakati kuliko utaratibu huu wa kuchimba na kuacha.

Kuna sehemu zingine zinaonekana korofi hata zikikarabatiwa mara nyingi iwezekanavyo hazichukui muda kuharibika ni bora itumike njia nyingine kudhibiti kuharibika mara kwa mara.

Kuna barabara ambazo zinapita kwenye maeneo yenye asili ya chemichemi ya maji ambazo kila zikikarabatiwa hazichukui muda mrefu zinaharibika. Barabara hizo zimepatiwa ufumbuzi kwa kutengenezwa kwa zege na sasa zimedhibitiwa haziharibiki tena.

Ni vyema utaratibu uliotumika kuzitengeneza barabara hizo ufanyike pia kwa zilizo korofi ili kuondokana na kero hiyo inayojitokeza mara kwa mara.

Ni bora kutumia gharama kubwa na ya mara moja kutengeneza barabara yenye ubora na inayodumu kuliko kukarabati kwa gharama nafuu ambayo itakugharimu kila baada ya mwezi kurudia kufanya ukarabati.

Barabara bora huokoa mambo mengi, huokoa vyombo vinavyopita kutoharibika, huepusha ajali za mara kwa mara na vile vile husaidia kuleta maendeleo.

Fedha ambayo ingetumika kufanya ukarabati wa mara kwa mara, itasaidia kufanya miradi mingine ya maendeleo kwa faida ya wananchi wanaoishi katika maeneo hayo.

Pia barabara nyingi zinakosa ubora kutokana na ukosefu wa mifereji ya kupitishia maji ya mvua na kusababisha kuharibika haraka.

Kama barabara zote zingejengwa kwa viwango vinavyotakiwa kero hii ya mashimo ingebaki historia na fedha hizo zingetumika kwenye mahitaji mengine.

Kuna barabara za mitaa ambazo zilitengenezwa tangu enzi za ukoloni, lakini mpaka leo zipo kwasababu zilitengenezwa kwa viwango.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Sabato Kasika

### Muungwana Lazima Nilonge

## TLP mjitafakari, mmalize mgogoro

**MIGOGORO** ya uongozi ndani ya vyama vya siasa imekuwa ni kama sehemu ya maisha hali ambayo isipopatiwa ufumbuzi, huenda itakwamisha demokrasia ndani ya vyama hivyo na pia kitaifa.

Baadhi ya vyama kama NCCR- Mageuzi, CUF na TLP, kwa nyakati tofauti vimepitia sintofahamu hiyo, ambayo inafaa kuwa somo kwa viongozi wa vyama hivyo, ili wachukue hatua za kuimaliza na kuikwepa.

Kwa sasa mgogoro unaofukuta, ni wa Chama cha TLP ambao ulianza mwanzoni mwa mwaka huu, wakati wa mchakato wa maandalizi ya uchaguzi wa kumpata mwenyekiti wa taifa.

Hadi sasa chama hicho hakijafanya uchaguzi, huku sababu za msingi ya kutofanyika zikidaiwa hazieleweki, hali ambayo imesababisha kuwapo kwa mgogoro wa kiongozi.

Mgogoro huo umefikishwa katika Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa, huku tuhuma zikielekezwa kwa Katibu Mkuu wa chama hicho, Richard Lyimo kuwa ndiye anayekwamisha uchaguzi huo.

Sababu kubwa inatajwa kuwa katibu mkuu huyo anataka kuchaguliwe kuwa mwenyekiti wa taifa na kwamba anahisi kuwa hawezi kuchaguliwa, hivyo anaona ni bora uchaguzi usifanyike kuliko akose nafasi hiyo ya uongozi.

Lakini yeye anakana na kufafanua kuwa hakuna ukweli wowote, bali sababu kubwa za kuahirisha uchaguzi huo, ni kwamba chama hakina pesa za kuandaa uchaguzi hadi hapo baadaye.

Kwa ujumla ni kwamba, kila upande unatoa sababu kuhusu kuwapo kwa mgogoro huo, lakini ni vyema pande zinazosuguana zikakutana katika meza ya mazungumzo zikamaliza mgogoro huo.

Ikumbukwe kuwa, migogoro ya kiuongozi ndani ya vyama vya siasa ni kikwazo cha demokrasia, kwani haviwezi kupiga hatua kwenda mbele badala yake inasababisha virudi nyuma.

Ninadhani wanaovutana ndani ya TLP, wangeacha demokrasia ichukue nafasi yake katika uchaguzi huo, ili yule ambaye wajumbe wa mkutano mkuu wanamtaka, wamchague kuongoza chama hicho.

Kwa kawaida, uhai wa chama chochote cha siasa ni kufanya kazi ya siasa, kwani kinyume chake ni hakiwezi kupata wanachama na kujikuta kinafutika au kuzusha migogoro ya kiuongozi.

Vilevile, lengo la chama cha siasa ni kushika dola, ili kitekeleza sera na ilani yake ya uchaguzi baada ya kuunda serikali, hivyo ni muhimu kifanye kazi kujitangaza kwa wananchi.

Njia ya kujitangaza ni kupitia mikutano ya hadhara kuanzia mijini hadi vijijini, kwa njia hiyo kinaweza kuenea nchi nzima bila kuwa na hivyo kuungwa mkono katika uchaguzi.

Bila kuwa ni mbinu kama hiyo na nyingine, si rahisi kuongeza wanachama au kujenga mtandao katika maeneo yote ya nchi, kwani ni muhimu chama kuwa na matawi, kufanya vikao kwa mujibu wa katiba.

Lakini kwa mgogoro unaoendelea ndani ya TLP, ni wazi chama hakiwezi kufanya kazi ya siasa, hadi hapo viongozi wake watakapokubali kukaa meza moja ili kumaliza tofauti zao zinazokwamisha uchaguzi.

Pamoja na hayo, ingependeza pia kama Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa itaingilia kati mgogoro huo na kuupatia ufumbuzi, ili chama kipate mwenyekiti wake wa taifa.

Ninadhani Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa bado inalo jukumu la kusuluhisha mgogoro huo na kuhakikisha chama hicho kinaendesha shughuli zake za kisiasa kuliko kilivyo sasa.

Demokrasia na uongozi wa pamoja vinapokosekana ndani ya chama, inazuka migogoro ya kiuongozi kama huo uliokikumba chama cha TLP, hivyo ingependeza iwapo chama hicho kitarudishwa kwenye mstari.

HABARI KITAIFA

# Samia awatua ndoo kichwani wanawake Morogoro

**Na Joseph Mwendapole**

NAIBU Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi, amempongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutoa kiasi kikubwa cha fedha za kutekeleza miradi mbalimbali ya maji inayokwenda kuwatua ndoo kichwani wanawake wa Mkoa wa Morogoro.

Aliyasema hayo juzi alipotembelea mradi wa maji wa Magadu mkoani hapa, inayotekelezwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (MORUWASA), ambayo itakuwa msaada mkubwa kwa wanawake wa mkoa huo.

Pia Naibu Waziri aliipongeza sekta ya maji mkoani humo kwa ushirikiano mkubwa katika usimamizi wa miradi ya maji na utunzaji wa vyanzo vyake.

Mahundi alitembelea na kukagua mradi wa maji wa magadu utakaonufaisha wananchi takribani 23,000 wa maeneo ya kata hiyo.

Aliwasisitiza wananchi kutunza miundombinu na vyanzo vya maji ili kuufanya mradi huo wa Magadu kuwa endelevu kwa vizazi vijavyo.

Naye Mkuu wa Wilaya Morogoro, Rebeca Nsemwa, alimpongeza Rais Samia na watendaji wake wa Wizara ya Maji kwa kazi kubwa wanayoifanya hasa kwa kuwapatia maji wakazi wa mkoa huo.

Mbunge wa Jimbo la Morogoro Mjini, Abdulaziz Abood, aliipongeza Wizara ya Maji kwa kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa asilimia 100.

Mkurugenzi wa MORUWASA, Mhandisi Tamim Katakweba alisema, ujenzi wa mradi huo uko katika hatua za mwisho na unarajiwa kuanza kuhudumia wananchi kuanzia mwezi Julai, mwaka huu.

Alisema MORUWASA inatekeleza miradi mingine ya muda mfupi itakayowezesha Manispaa ya Morogoro kupata huduma ya maji kwa asilimia 96 ifikapo 2025.

Mahundi pia alitembelea mradi wa kuhifadhi chanzo cha maji mto Tangeni, unaotekelezwa na Bodi ya Maji Bonde la Wami/Ruvu na kupongeza juhudi za utunzaji na uhifadhi wa vyanzo vya maji.

Aliwataka watendaji kuendelea kufanya vizuri hususani kupanda miti rafiki kwa maji ili kukifanya chanzo hicho kidumu.

Akizungumza wakati wa ukaguzi wa chanzo hicho, Mkurugenzi wa Bonde la Wami Ruvu, Mhandisi Elibariki Mmassy, alisema kuwa Bodi imetekeleza ujenzi wa uzio katika vidaka maji 13 vinavyotumiwa na MORUWASA pamoja na RUWASA-Morogoro.

Mmasy alisema bodi imeweka alama za kudumu (beacon) na mabango ya makatazo ikiwa sehemu ya utunzaji wa chanzo hicho cha maji. Alisema Bodi ya Wami/Ruvu imeendelea kufanya utafiti wa maeneo ya hazina ya maji chini ya ardhi pamoja na kuyatangaza maeneo hayo kuwa eneo tengefu la vyanzo vya maji.

Akizungumza kwa niaba ya sekta ya maji, Meneja wa RUWASA Mkoa wa Morogoro, Sospeter Lutanjo, alimshukuru Naibu Waziri kwa ziara yake na kusisitiza kuwa umoja wa sekta ya maji Morogoro ni kielelezo cha uchapakazi wa Wizara ya Maji kutoa huduma kwa wananchi.




Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi Zanzibar, Abdalla Hussein Kombo (katikati), Ofisa Biashara Mkuu Benki ya CRDB, Boma Raballa (wa pili kushoto), Mkurugenzi wa Wateja Wadogo na Wakati wa benki hiyo, Bonaventura Paul (wa pili kulia), Mkuu wa Kitengo cha Huduma kwa Wateja, Yolanda Uriyo (kushoto) na Meneja Mwandamizi Kitengo cha Biashara, Agnes Kisinini, wakiwa pamoja na baadhi ya wateja wa benki hiyo na wajasiriamali katika hafla maalum ya kuadhimisha Siku ya Wajasiriamali Duniani jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanawake wakulima wakutana kupinga ukatili, unyanyasaji

**Na Zuwena Shame,** BABATI

UMILIKI wa ardhi na unyonyaji wakati wa kuuza mazao ya kilimo ni changamoto zinazochangia ukatili wa kijinsia nchini kwa mkulima mdogo mwanamke na kuongeza umaskini.

Wanawake 130 walioshiriki katika mkutano wa kwanza wa kikanda wa wanawake wakulima wadogo wanachama wa MVIWATA kutoka mikoa ya Manyara, Dodoma, Kilimanjaro, Tanga na Arusha, walisema.

Pia walisema baadhi ya mila na desturi haziruhusu mwanamke kurithi au kumiliki ardhi suala linalomsababishia mwanamke changamoto ya kutokuwa na uhuru wa kuendeleza kilimo na kujipatia manufaa na pia kutokuwa na uamuzi wa kuuza mazao yao wenyewe.

Walisema kawaida kwa mwanamke kulima katika shamba la familia na kutumia nguvu kazi yake, lakini inapofika wakati wa kuuza mazao hawashirikishwi kufanya uamuzi wa bei na hata kutumia fedha zitokanazo na mauzo.

"Tumekuwa waathirika wakubwa katika suala la kumiliki ardhi, tunalima kwenye ardhi tusizozimiliki na hatimaye wakati wa kuuza mazao hayo sokoni tunakosa kauli katika kupanga bei na kwa habari mbaya zaidi, tunapangiwa na wenza wetu," alilalamika mmoja wa wanawake hao.

Aidha, walisema changamoto ya umilikishwaji wa ardhi kwa mwanamke au mtoto wa kike imetokana na baadhi ya mila na desturi zinazopinga mtoto wa kike kumiliki ardhi zikidai ni mwiko.

Walisema kuwa ni wakati sahihi sasa kwa wanawake wakulima wadogo nchini kupaza sauti kwa kujua haki zao linapokuja suala la kumiliki ardhi na nafasi yao katika kutunza jamii na rasilimali zake.

"Ni muda mwafaka sasa kuungana na kuwa na sauti moja kupinga ukatili wa kijinsia katika kilimo. Wanawake tuwe na sauti moja kupinga hili kwani sisi ndiyo waathirika wakubwa na ndiyo watunza familia wakubwa," alisema Asia Mmbonde, mwanachama wa MVIWATA.

Pia changamoto ya ukosefu wa mikopo, masoko ya mazao, pembejeo zinazoendana na mahitaji yao na kukosa ruhusa kwa wenza wao wanapohitaji kushiriki mikutano au makongomano mbalimbali yanayogusia masuala ya wanawake na maslahi yao kwa ujumla.

Mkuu wa programu kutoka taasisi ya MVIWATA, Theodora Pius, alisema mkutano huo wa kwanza kikanda ni utekeleaji wa maazimio ya mikutano mikuu ya wanawake kitaifa likiwa moja ya mapendekezo ya wajumbe katika mikutano hiyo kuwakusanya wakulima wanawake wadogo na kujadili changamoto zao na kusambaza elimu ya kupinga ukatili dhidi yao.

Alisema kuwa tangu kuanzishwa kwa taasisi hiyo, wakulima wadogo wanawake wamekuwa mstari wa mbele na kuweka jitihada taasisi inaendeshwa ipasavyo na kwa usawa ili kufikia malengo yake.

Naye Lina Woiso kutoka Taasisi ya La Via Campesina, kanda ya Kusini na Mashariki, aliwataka wanawake hao kuifahamu dhana ya ufeminia wa wakulima wadogo katika mapambano na ukombozi wao.

Lina alisema ufeminia wa wakulima wadogo haujengwi na wanawake pekee bali mavuguvugu ya wakulima wadogo kwa ujumla wake kwa sababu dhana hiyo inalenga kubomoa mizizi ya unyonyaji kwa tabaka zima la wavuja jasho ambayo pia imejikita chini kabisa kwenye jamii za wavuja jasho ambapo waathirika wakubwa ni wanawake na hivyo kuhitaji mshikamano wa jamii kwa jumla.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# TIRA yaeleza usumbufu wanaostahili kulipwa bima

**Na Maulid Mmbaga**

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA), imesema imebaini baadhi ya kampuni za bima haziwalipi wananchi stahiki zao kwa wakati wanapopata tatizo linalostahili kuhudumiwa kisheria.

Kamishna wa Bima, Baghayo Saqware, alisema hayo juzi wakati wa mkutano wa mwaka uliokutanisha mawakala wa bima Tanzania kwa lengo la kujadili mwenendo wa utendaji wao wa kazi.

Alisema walibaini uwapo wa changamoto hiyo baada ya kufanya mikutano mkoani Dodoma, Mbeya, Mwanza, Pemba na Zanzibar kwa ajili ya kusikiliza na kupokea malalamiko ya wananchi kuhusu huduma ya bima.

"Hiyo imekuwa ni changamoto kubwa na imetusaidia sisi kuboresha kanuni zetu na hivi karibuni tulitoa kanuni ya viwango vya kulipwa kwa mtu wa tatu (third part payment) ambaye amepata ajali kwenye vyombo vya moto, jambo hilo limesaidia kuweka muda maalum wa kila jambo wakati wa kulipa," alisema Saqware.

Kadhalika, changamoto nyingine ni wananchi wengi hawana bima na kudai bima za watu wengine, akisema kuwa kuna bima ya aina tatu kwenye magari ikiwamo ya gari, ya dereva na ya gari ikimuumiza mtu mwingine, malalamiko mengi wanayapata kwa watu ambao hawana magari ambao wameumizwa.

Kwa mujibu wa kamishna huyo, endapo mtu hana bima yake, changamoto zinakuwapo anapopatwa na tatizo kwa kuwa lazima wahakikishe mtu kagongwa na gari lipi, wapi na mahakama ithibitishe kwamba aliyegonga ndiye ana makosa.

"Rai yetu kwa Watanzania ni kununua bima yake mwenyewe, ukiwa na bima yako ya safari na ukapata tatizo huwezi kuchukua muda mrefu kupata haki yako, lakini kama utadai kwasababu ulikuwa ni abiria ina utaratibu wenye mlolongo ambao tunajaribu kuufupisha na hiyo ndiyo changamoto kubwa," alisema Saqware.

Hata hivyo, alitoa wito kwa kampuni zote za bima kufuata utaratibu vinginevyo sheria itachukua mkondo wake na kwamba wameelekeza kampuni zote waanze kutumia lugha ya Kiswahili kwenye mikataba ya bima.

Vile vile, aliwapongeza mawakala zaidi ya 1,000 wenye leseni kwa uthubutu wa kuanzisha huduma za bima nchini, akieleza kuwa wanawasaidia katika kuwahudumia Watanzania na waendelea kusikiliza changamoto zao na kuzitatua.

Mwenyekiti wa Chama cha Mawakala wa Bima Tanzania, Sai Daudi, alisema kampuni za bima ziko chache, lakini kuna mawakala walioenea nchi zima na kwamba wamekutana kupeana mbinu za namna ya kutoa huduma kwa ubora.

"Tuko kwenye mkutano kuangalia changamoto zinazotukabili katika kufikisha huduma kwa wananchi kama serikali inavyotaka kwamba angalau soko liwafikie Watanzania kwa asilimia 50, tunajaribu kupeana mbinu namna gani tuwahudumie watu kwa ufanisi zaidi," alisema Daudi.



Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea mkoani Lindi, Mohamed Moyo (kulia), akikagua ujenzi wa madarasa mapya katika Shule ya Msingi Kiegei juzi, inayojengwa kupitia fedha za mradi wa Boost. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# PEPFAR yaendesha kambi vijana uelewa VVU

**Na Christina Mwakangale**

SHIRIKA la Mulika Tanzania kwa kushirikiana na Mpango wa Dharura wa Rais wa Marekani wa kukabiliana na Ukimwi (PEPFAR), wameendesha kambi ya siku nne ya vijana wenye umri kuanzia miaka 15 hadi 25, kuwapatia uelewa namna ya kukabiliana na maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi (VVU) na mbinu za kujikwamua kiuchumi.

Mkurugenzi wa shirika hilo, Hussein Melele, akizungumza mwishoni mwa wiki, kwenye kambi iliyofanyika Wilaya ya Kigamboni, Dar es Salaam, alisema lengo la kambi hiyo 'JIKWAMUE Youth Camp' ni kuwapa elimu vijana hasa mabinti wa kike, ambao ni waathiriwa wakubwa wa VVU.

"Njia ya kufanya kambi na kutoa elimu ni rafiki, kwa kuwa vijana huwa huru, wataongea, kuzungumza, kuuliza maswali yanayowatatiza. Watajifunza ambavyo hawavifahamu. Taifa letu asilimia kubwa ni vijana, tuwalinde."

"Vijana wanapaswa kuwa mbali na magonjwa, tunawapa elimu ya afya ya uzazi, mtaji wa kwanza wa kijana ni afya. Ujana ni muda wa mpito, wanatakiwa wajitambue na kuwa na maamuzi sahihi. Watunga sera, wadau wa maendeleo wawaunge mkono vijana, ili wainuke kiuchumi," alisema Melele.

Alisema mradi huo wa uelimishaji utawafikia vijana 60 kutoka wilaya mbili za mkoani humo, Kinondoni na Kigamboni, akisema wanawaandaa vijana hao kuwa wakufunzi kwa wenzao pia wakiwaunganisha na vituo vya afya sehemu wanakoishi.

Inspekta Blandina Ndunguru kutoka Kituo cha Polisi Chang'ombe, Dawati la Jinsia na Watoto, akiwa mmoja wa wakufunzi kwenye kambi hiyo, alisema elimu aliyoitoa ni kuhusu ukatili wa kijinsi ambao kwa sasa umekuwa kinyume na kuwakumba zaidi watoto wa kiume.

Alisema awali matukio ya ukatili yalijitokeza kwa watoto wa kike, tofauti na sasa zaidi yanawakumbuka watoto wa kiume, huku wakilawitiwa na ukubwani kugeuka kuwa mashoga.

"Watoto wa kiume unyanyasaji unaanza tangu wakiwa chini, chekechea, shule za msingi na wazazi hawawi makini wanajikita katika zaidi kwenye kujitafutia, badala ya malezi. Unakuta mtoto amekwishakuwa shoga ndio mzazi anashtuka," alisema Inspekta Blandina.

Alisema kwa uzoefu wake inaonekana wazazi wanajikita zaidi kwenye kutafuta kipato, wakitoka majumbani mwao asubuhi watoto wao wakiwa wamelala na kurejea usiku, muda ambao pia huwakuta wamekwishalala.

"Elimu watoto hawapati, siku hizi hata vitendo vya usagaji vimeongezeka kwa kuwa utakuta vibinti vidogo ni 'tomboy'. Walianza kufanya vitendo hivi wakiwa wadogo kabisa, mbaya zaidi wakiwa wakubwa wao wanawahonga wanaume, wanawapa magari, wanamakundi wanahamasisha watu waungane nao," alisema.

Kadhalika, Inspekta Blandina alisema pia kuna changamoto ya uendeshaji kesi na kuzipatia ushahidi, kwa kuwa kesi zinafunguliwa na hukwamia kwenye kipengele cha ushahidi mahakamani, alisema:

"Wazazi wanauza utu wa watoto wao, wanajipatia pesa, wakishafanyiwa unyanyasaji watoto wao wanajua watalipwa fidia labda laki mbili. Wazazi walee watoto wao, unyanyasaji umekithiri. Pia watoto wa kike wanajibakisha, yaani wanajipeleka katika nyumba za wanaume halafu wanasema wamebakwa."

## Atoweka, wasiofahamika watuma SMS kumshikilia

**Na Mwandishi Wetu**

FAMILIA ya Salha Lucas, inayoishi Mbezi Mwisho Dar es Salaam, imepotelewa na mtoto wao kwa wiki mbili na kupigiwa simu na mtu asiyefahamika kuwa anamshikilia.

Akizungumza na Nipashe jana, mama mzazi wa kijana Salha, alisema mwanawe Revocatus Njau (17), anayesoma Sekondari ya Kibaha Miembe Saba, mkoani Pwani, alitoweka Jumanne iliyopita Juni 13.

"Aliaga kuwa anakwenda kucheza mpira uwanja wa jirani na marafiki zake baada ya chakula cha mchana. Nimekuwa na hofu zaidi kwani baada ya kumtafuta jioni na usiku kwa marafiki na kuulizia kwa ndugu nilipata ujumbe wa simu kuwa amekamatwa na polisi," alisema Salha.

Aliongeza kuwa ilipofika saa 6:15 usiku alipata ujumbe kutoka namba 0686-288505 inayosema 'mwanao tumemkamata yuko kituo cha Stendi ya Polisi Mbezi Magufuli.'

"Nilipompigia simu kuwa Revocatus (pichani), amefanya kosa gani hakujibu. Nikapiga mara kadhaa ikiwa haipokelewi na mwisho 'ameniblock' kila nikipiga inatumika, akimpigia mtu mwingine inapokewa na nikizungumzia suala la mtoto anakata," alisema.

Aliongeza kuwa alikwenda kituo cha Magufuli, lakini polisi kwa mshangao walisema hawafahamu taarifa hizo na walipoita jina lake hakuonekana wala kusikika.

Nipashe iliwasiliana na mwenye simu hiyo iliyosajiliwa kwa jina la Semen Shabani na kusema kuwa hajatuma ujumbe wala hamfahamu Revocatus.

Alijitambulisha kwa jina la Ramadhani Abdallah na kwamba kitambulisho kilichosajilia laini yake ni cha bibi yake mwenye jina la Semen Shaban na kwamba alikitumia kwa sababu ni mwanafunzi hana utambulisho.

Alipoulizwa kama kuna vijana waliomba simu yake na kuitumia bila yeye kujua, alikataa akisema muda wote alikuwa nayo na anashangaa kuhusishwa na suala hilo.

Salha mzazi wa Revocatus, alisema polisi wameahidi kufuatilia suala hilo kwenye mamlaka za usajili wa laini za simu.

Aliomba atakayemwona Revocatus awasiliane na familia kwa namba 0658-734445 au 0715-580346 kwa Salha Lucas au awasiliane na kituo cha polisi na kwamba tukio hilo limeripotiwa na kufunguliwa faili MBT/RB/3207/2023.





## Majaji 16 SADC kujadili upatikanaji wa haki

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

MAJAJI 16 kutoka nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), watakutana jijini Arusha, kujadili masuala mbalimbali ikiwamo upatikanaji haki kwa wakati.

Mkutano huo uliopangwa kufanyika Oktoba mwaka huu, pamoja na mambo mengine utajadili namna bora ya kuondoa vikwazo vya kibiashara katika nchi hizo.

Akizungumza jana katika kikao cha sekretarieti ya Jukwaa la Majaji Wakuu wa SADC, Jaji wa Mahakama ya Rufani (Tanzania), Ignas Kitusi, alisema mkutano huo utafanyika kuanzia Oktoba 23 hadi 28 mwaka huu.

"Tunatarajia kukutana majaji wakuu kutoka nchi 16 na tunaimani kuwa tutashirikishana mengi kuhusu upatikanaji wa haki hususani katika Mahakama. Lengo ni kuharakisha upatikanaji wa haki ili wananchi waweze kuendelea na shughuli za kibiashara,"alisema Kitusi.

Aidha, majaji hao watajadili njia bora ya kutatua vikwazo vya biashara vinavyotokana na mkwamo wa haki au mashauri.

Kwa mujibu wa Jaji Kitusi, mada nyingi zitajadiliwa katika mkutano huo ikiwamo utatuzi wa migogoro ya biashara katika nchi za SADC.

Mbali na kushirikishana uzoefu, pia watapata nafasi ya kutembelea hifadhi za taifa na vivutio mbalimbali vya utalii. Mgeni rasmi katika mkutano huo ni Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Awali, Mkuu wa Sekretarieti hiyo, Nyimbiri Sangwani, alisema kupitia mkutano huo watashirikishana uzoefu wa namna bora ya kuendesha mashauri, huku wakitarajia kujifunza kutoka nchi washiriki.

Mkutano huo ni wa 20, tangu kuanzishwa kwa umoja huo mwaka 2003.

# Wazazi, walezi watajwa kuhusika aina mpya ukatili

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MKUU wa Dawati la Jinsia na Watoto wa Jeshi la Polisi, Mkoa wa Kilimanjaro, Mrakibu Msaidizi (ASP) Asia Matauka, amesema aina mpya ya vitendo vya ukatili hivi sasa ni ule unaohusisha wazazi au walezi, kurithisha watoto visasi kwenye migogoro ya ardhi na migogoro ya ndoa.

Aliyesema hayo jana wakati akizungumza na wafanyabiashara wadogo na wachuuzi wa Soko la Mitumba la Kumbukumbu ya King George, maarufu Meimoria, Matauka, alisema migogoro mingi inayoripotiwa inapochunguzwa hubainika imezaa visasi ambavyo watoto wamerithi kwa wazazi wao.

Alikuwa akitoa mada jana kuhusu vitendo vya ukatili katika kampeni maalum iliyoandaliwa na Shirika la TUSONGE CDO, linalotekeleza Mradi wa Afya Yangu, Mtaji Wangu.

"Nimeona kesi nyingi ni za viamba na ndoa. Wazazi wanagombana na mgogoro ule unageuka visasi hadi kwa watoto. Na visasi hivyo vinasababisha kufanyika vitendo vya ukatili, mtoto au watoto wakidhani kwamba wanalipiza kile ambacho wazazi wao walifanyiwa. Hii ni mbaya na haikubaliki katika jamii yetu," alisema.

Katika kampeni hiyo, Shehe wa Msikiti wa Mfumuni wa Baraza la Waislamu Tanzania (BAKWATA), Bashiri Mahalo, alisema kuibuka kwa ndoa za jinsia moja ni kutengeneza hasira au kadhia dhidi ya Mwenyezi Mungu.

"Unapofanya ukatili unamwathiri mtu kiasi kikubwa sana, lakini ukatili huo huo unaofanya, kwa mfano kuingiliana kinyume na maumbile, una athari kwa anayefanya na anayefanyiwa.

"Kukosekana kwa maadili na kukosa subira, kunamsababishia mtu kuingia kwenye mambo ambayo hayafai katika jamii. Kama jamii yetu watu watakuwa wanaoana wa jinsia moja, yaani mwanaume kwa mwanaume na mwanamke kwa mwanamke, kwa akili ya kawaida ambayo huitaji kwenda shule taifa linapotea hapo.

"Hili la mapenzi ya jinsia moja kulikubali ni kuangamiza taifa, sio kwamba viongozi wav dini tunapiga kelele kwamba jambo hili limepita mipaka ya kimungu lakini ni kwenda kulizika taifa. Tuungane sote kwenye jambo kama hili bila kujali dini, kabila, tuungane kwenda kulikomboa taifa," alisema.

Kuhusu maambukizi ya ugonjwa wa corona, Mratibu wa Mradi wa Afya Yangu, Mtaji Wangu, Lawi Msemwa, alisema kulingana na taarifa ya Wizara ya Afya, kwa sasa ugonjwa huo siyo kwamba umepotea bali bado upo. "Wote tunafahamu kuwa corona ni janga la kidunia na kila mmoja ameathiriwa nao kwa namna moja au nyingine. Kila mtu anakumbuka namna mwaka 2020 tulivyokuwa na hali ngumu sana lakini leo tuna unafuu.

"Kwa sababu tuna uwezo wa kuendelea kufanya shughuli zetu kama kawaida na tumeendelea kupata kipato wakati huo huo afya zetu zikiendelea kuimarika na kuwa salama zaidi, lakini kulingana na Wizara ya Afya, kwa sasa corona siyo kwamba huu ugonjwa umepotea bali upo.

Zaidi alisisitiza: "Na sisi kama wanajamii tuna jukumu la kuhakikisha anaendelea kuchukua tahadhari ya kuendelea kupambana na huu ugonjwa.



Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza mkoani Tanga, Dk. Jumaa Mhina (wa pili kushoto), akizungumza na waandishi wa habari katika viwanja vya ofisi za halmashauri hiyo juzi, wakati akiipongeza serikali kwa kuleta fedha za miradi ya maendeleo katika sekta mbalimbali kwa kipindi cha miezi sita kiasi cha zaidi ya Sh. bilioni 9. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# DC ahamasisha wanawake kupima ubavu na wanaume

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKUU wa Wilaya ya Arusha, Felician Mtahengerwa, amewashauri wanawake kutobweteka na nafasi za viti maalum, badala yake wahamasike, kujitokeza 'kupimana ubavu' na wanaume wakati wa uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu ujao.

Mtahengerwa aliyasema hayo jana jijini Arusha, wakati akifunga mradi wa uhimizaji demokrasia uongozi bora na maendeleo jumuishi.

Mradi huo unatekelezwa na Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (TAWLA) kwa kushirikiana na Shirika la Vijana Tanzania (TYC) na Taasisi ya We Effect.

Katika hotuba yake, Mtahengerwa alisema ni muhimu makundi hayo kujitokeza kushiriki katika shughuli za maendeleo ikiwemo chaguzi mbalimbali.

"Miongoni mwa vitu ambavyo vilikuwa haviwezekani kwenye jamii kwa sasa vinawezekana ilikuwa vigumu sana mwanamke kusimama akaomba kura, akapigiwa lakini kutokana na michango ya wadau na serikali, wameweza kuhamasisha wanawake na vijana.

"Kwa sasa wanawake wana uwezo wa kusimama kwenye majukwaa wakashindana na wanaume na wakatoboa, zamani tulikuwa tunawatengea nafasi za viti maalum sasa wanaingia wanapambana na wanashinda, hivyo muendelee kujitokeza kuwania na kushiriki kwenye masuala ya maendeleo," alisema.


Kabla ya kufunga mradi huo, Mratibu wa Programu wa TAWLA, Isabella Nchimbi, alisema mradi huo wa miaka mitatu ulitekelezwa katika majimbo 13 yaliyopo mikoa ya Arusha, Tanga na Mwanza.

Alisema tangu kuanza kwake mwaka 2020, wamefanikiwa kufikia watu zaidi ya milioni 1.5.

Alisema lengo la mradi huo uliofadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU) ni kuhakikisha wanawake na vijana, wanashiriki kwa wingi katika nafasi za uongozi, ambao umetekelezwa kwa vipindi vitatu ambavyo ni kabla ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2020, wakati wa uchaguzi na baaada ya uchaguzi, ambapo walitoa elimu ya uraia na mpigakura.

Mmoja wa wanufaika wa mradi huo, ambaye ni Diwani wa Viti Maalum, Muheza mkoani Tanga, Fatuma Kweka, alisema kupitia mradi huo alishiriki na kuwania nafasi hiyo, ambapo kabla hakuwa na ujasiri wa kugombea.

Alisema: "Mimi ni mnufaika wa moja kwa moja wa mradi huu, mafunzo tuliyopewa kabla ya uchaguzi mkuu wa 2020 yalinijengea uwezo, kujiamini na nikaamua kugombea na nikashinda, hivyo ni muhimu kuwapo miradi kama hii inasaidia jamii kutambua haki na wajibu wao."





# Huduma ya mlango kwa mlipa kodi yarahisisha upatikanaji TIN

**Na Alex Sayi,** SIMIYU

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) Mkoa wa Simiyu imesema uanzishwaji wa mfumo wa huduma ya mlango kwa mlipakodi imerahisisha upatikanaji wa Namba ya Utambulisho wa Mlipakodi (TIN) na kusaidia kuboresha shughuli za utoaji huduma kwa wananchi.

Hayo yamebainishwa juzi na Ofisa Elimu na Huduma TRA, Mkoa wa Simiyu, Benjamini John wakati akizungumza na Nipashe.

Alisema kuwa huduma hiyo ya kimtandao imeondoa usumbufu kwa wananchi kwani kwa sasa huitaji kupanga foleni katika ofisi za TRA ili kupata namba hiyo.

John alisema kuwa kumekuwa na ongezeko la walipa kodi mkoani humo kutokana na wepesi na urahisi uliopo kwa sasa kwa wafanyabiashara kwa kupata TIN kwa njia ya simu janja.

"Tunajitahidi kuandikisha tunapata walipa kodi wapya ambako tangu kuanzishwa kwa mfumo huu wananchi wamekuwa wakijiandikisha kwa wingi hadi kufikia Mei, 2023 tumeandikisha walipa kodi zaidi ya 1,000 tofauti na hali ilivyokuwa kwa mwaka jana," alisema John.

Aliongeza kuwa: "Jukumu la TRA siyo kukusanya kodi tu vilevile tunatoa elimu ambako kwa sasa uelewa umeongezeka kwa wananchi wameanza kulipa kodi kwa hiari hali inayoisaidia serikali kuendelea kuboresha miundombinu ya barabara, umeme na sekta ya viwanda haya yote yamechochea ongezeko la walipa kodi wapya."

Meneja TRA Wilaya ya Maswa, Lucius Theonesti, alisema kuwa ulipaji kodi kwa hiari kunaipunguzia gharama TRA ukusanyaji wa mapato, huku akiwaomba baadhi ya wafanyabiashara wanaokwepa kulipa kodi na kufunga biashara zao waone umuhimu wa kulipa kodi kwa ajili ya maendeleo ya taifa.

"Nawashukuru wafanyabiashara wanaolipa kodi kwa hiari, wilayani hapa ingawa kuna baadhi ya wafanyabiashara wanaokwepa na wanawakatisha tamaa wanaolipa, tunajua walipa kodi wakiwa wengi wanapunguza mzigo wa ukusanyaji wa mapato ya nchi," alisema Theonisti.

Diwani wa Kata ya Jijabirishi wilayani hapa, Daudi Lubinza, alizungumzia suala la baadhi ya wafanyabiashara katika kata yake kudaiwa kukwepa kulipa kodi alisema kuwa suala hilo kwa sasa halipo kutoka na elimu inayoendelea kutolewa na mamlaka hiyo.




Meneja Mawasiliano na Uhusiano wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA), Yessaya Mwakifulefule, akizungumza na waandishi wa habari, wakati akitoa tamko la mamlaka la kutoutambua usajili wa chuo cha Tanzania Aviation College tawi la Mwanza mbele ya uongozi na wanafunzi, ambacho kimekuwa kikitumia usajili namba CAA/ATO/050 ulioisha muda wake tangu mwaka 2018 kitendo ambacho ni kinyume cha taratibu za usajili kama ulivyoainishwa katika Sheria ya Usafiri wa Anga, sura ya 80 na kanuni zake. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TAA yapewa ujenzi jengo la abiria uwanja wa ndege

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, Amos Makalla, amesema mchakato wa ujenzi wa jengo la abiria la uwanja wa ndege mkoani humo tayari umekabidhiwa kwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Nchini (TAA).

Aliyasema hayo juzi wakati wa mkutano wa Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza kujadili hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Alisema kuwa ni dhahiri uwanja huo ulikosewa katika ujenzi wa awali hivyo kuilazimu ofisi yake kuukabidhi kwa TAA.

Makalla alisema kuwa mradi huo ni jicho la Mkoa wa Mwanza na Kanda ya Ziwa kwa ujumla, hivyo kukamilika kwake kutasaidia Mwanza kuwa na uwanja wa kimataifa utakaopokea watalii na wageni mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi na kukuza uchumi wa mkoa.

Katika hatua nyingine Makalla aliitaka menejimenti ya Halmashauri ya Jiji la Mwanza kuhakikisha wafanyabiashara wa eneo la Mlango Mmoja wanalipa madeni ya kodi wanayodaiwa na kuhakikisha wanapitia mikataba na nyaraka zinazowasilishwa.

Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana, Amina Makilagi, aliahidi kuhakikisha hoja zote za CAG ambazo hazijajibiwa zinakuwa ajenda katika vikao vyote vya ulinzi na usalama ili CAG atakaporudi katika vikao vijavyo hoja ziwe zimepungua au zimejibiwa zote.

Kaimu Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Ndani, Waziri Shabani, alisema anatambua ushirikiano alioupata kwa madiwani na wafanyakazi wote wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza ili kuhakikisha hoja za CAG zinakamilishwa kwa mujibu wa sheria.

Naye Mstahiki Meya wa Jiji la Mwanza, Sima Constantine, alisema kuwa kwa kadri siku zinavyozidi kwenda wanamatumaini kuwa halmashauri hiyo ipo siku itasimama bila kuwa na hoja hata moja kwani weledi na utendaji kazi wa watumishi unaendelea kuimarika.

# CCM Tarime yaomba ushirikiano na vyama vya upinzani

**Na Waandishi Wetu**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Kata ya Itirinyo, wilayani Tarime mkoani Mara kimeomba ushirikiano kutoka vyama vya upinzani katika utekelezaji na ulinzi wa shughuli za kimaendeleo zinazoendelea kutekelezwa na viongozi wa ngazi ya juu.

Ombi hilo lilitolewa juzi na Diwani wa Kata ya Itirinyo, Shadrach Muruga, wakati akitoa taarifa ya utekelezaji wa shughuli za maendeleo katika kipindi cha miaka miwili.

Alisema kuwa njia pekee ya kupiga hatua za haraka kimaendeleo ni kusaidiana kusukuma juhudi hizo mbele badala ya kuvuta nyuma kwa itikadi za kisiasa.

"Haijalishi wewe ni wa chama gani lengo ni kuleta maendeleo kwa Wanaitirinyo maana hata wewe ukipata ridhaa hiyo kwa muda wako tutakuunga mkono kwa lengo ni kujenga wala siyo kurudisha nyuma shughuli za kimaendeleo," alisema.

Alisema kuwa zaidi ya Sh. bilioni moja zimetumika katika miradi mbalimbali ya maendeleo katika kata hiyo huku baadhi ya fedha hizo zikitumika kukamilisha ujenzi wa matundu ya vyoo vya shule, vyumba vya madarasa na nyumba za walimu.

Akizungumza katika mkutano wa Baraza la Jumuia ya Wanawake (UWT) Wilaya ya Tarime, Mjumbe wa mkutano mkuu wa CCM, Daniel Chonchori, aliwataka viongozi na wanachama kusemea miradi inayotekelezwa kwa jamii.

Naye Mwenyekiti wa UWT Mkoa wa Mara na Katibu wa Siasa, Itikadi na Uenezi mkoani humo, Nansi Sesani, aliwaomba wanachama wa chama hicho kusimama pamoja katika kuhakikisha wanasimamia utekelezaji wa shughuli za kimaendeleo.

Wakati huo huo, Mwenyekiti wa UVCCM mkoani Shinyanga, Clement Mandinda, aliwataka wanafunzi wa vyuo vikuu mkoani Shinyanga kuwa wanyenyekevu na wenye nidhamu, lengo likiwa ni kulinda heshima ya chama hicho na kuwa kioo katika jamii wanakotokea.

Hivyo, aliwataka kuacha kuwa tegemezi kwa kuhakikisha wanafanya kazi kwa bidii na kujiinua kiuchumi pamoja na kuwa karibu na fursa zilizopo mkoani humo, kwamba serikali mkoani Shinyanga inaleta wawekezaji watakaoanzisha viwanda vidogo vidogo, kuinua uchumi wa mkoa.

**Imeandaliwa na Mathias Marwa (TARIME), Timothy Itembe (MARA), Neema Sawaka (KAHAMA)**



Ukurasa 12

**Siasa zinavyokoleza migogoro Kigamboni**



Ukurasa 13

Rais Dk. Samia akiwekeza kumwinua mama kila kona zinazoamua nchini




Ukurasa 14

**UASI WA WAGNER**

**Unavyoleta mkanganyiko vita vya Russia, Ukraine**


# siasa

JUMATANO JUNI 28, 2023

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe


KATIBA MPYA

# Chongolo aamsha mapya, huenda yajayo yakasikitisha, wadau wahofia haitakuwapo

**Na Sabato Kasika**

KATIBA mpya ni miongoni mwa vipaumbele vya Wizara ya Sheria na Katiba katika bajeti ya mwaka 2023/24, kama ambavyo Waziri wa Katiba na Sheria, Dk.Damas Ndumbaro anavyolidokeza bunge.

Wizara yake inaidhinishiwa Shilingi bilioni 383.61 bajeti ya mwaka huo kwa kazi zinazotarajiwa kuanza Julai mosi na kazi ya katiba mpya ikiwa ni namba moja.

Ndumbaro anaeleza kuwa wizara yake ina vipaumbele 30, lakini kuratibu mchakato wa katiba mpya ndilo jukumu muhimu na la kipekee katika mlolongo huo.

Wakati wizara ikiwa imeelezea uwekezaji kwenye mchakato huo, Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo, naye anakaririwa na vyombo vya habari akisema chama hicho ndicho kitakachoongoza mchakato wa katiba ya kisasa.

Katika katiba hiyo itaandaliwa kisasa na itatengenezwa kupitia mikono, uongozi, usimamizi na uratibu wa CCM na si vinginevyo.

Kauli hiyo imewaibua wadau mbalimbali wa mambo ya katiba na siasa, huku kila mmoja akitoa mtazamo wake na kushauri kama inavyowezekana.



Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo. **PICHA: BLOG CCM**

### CCM ISIHODHI

Katibu Mkuu wa Chama cha ACT-Wazalendo, Ado Shaibu, anasema mchakato wa kupata tume huru ya uchaguzi na katiba mpya, unapaswa kuwa shirikishi, wa wazi na jumuishi ukileta wadau wote muhimu na kwamba CCM isihodhi ili kuwapa Watanzania wote nafasi ya kuandaa kila wanachokitaka.

"Nimemsikia Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo, akisema mchakato wa kuandikwa kwa katiba mpya utasimamiwa na kuratibiwa na chama hicho. Hatutakubali hilo litokee," anasema Shaibu.

Anafafanua kuwa katiba inayotafutwa si ya CCM wala watu wachache au kikundi chenye mawazo ya aina moja bali ya Watanzania na kwamba inapaswa kupatikana kwa uwazi na ushirikishwaji wa makundi yote kwenye jamii.

"Ni muhimu tujifunze kilichokwamisha mchakato wa awali mwaka 2014. Somo la kwanza ni kutanguliza mbele maslahi ya vyama dhidi ya maslahi ya taifa," anakumbusha Shaibu.

Aidha, anasema ni muhimu vyama vyote vya siasa na makundi yote muhimu kwenye jamii yashirikishwe katika kujenga mwafaka wa kitaifa ili mchakato usikwame tena.

"Pamoja na hayo, narejea rai ya chama chetu ya kutaka kuandikwa upya kwa Sheria ya Uchaguzi ndani ya mwaka 2023 ili kuanzisha tume huru ya uchaguzi itayosimamia uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu ujao," anasema.

Aidha, anaitaka serikali iweke wazi lini mchakato wa katiba mpya utaanza, hasa hatua muhimu za kupitiwa upya kwa sheria ya mabadiliko ya katiba na sheria ya kura ya maoni.

Kuitishwa kwa mkutano wa majadiliano ya kitaifa kuhusu katiba na kuundwa kwa kamati ya wataalamu ya kuchambua maoni ya wadau na kuandika katiba pendekezwa itayopigiwa kura ya maoni.

### TAMBO ZA KISIASA

Mkurugenzi wa Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA), Bob Wangwe, akinukuu kauli ya Katibu Mkuu wa CCM anaifananisha na tambo za kisiasa na kwamba hazipaswi kuzingatiwa.

Anafafanua kuwa mchakato wa katiba hausimamiwi na chama cha siasa, Chongolo ni kama alikuwa anataka kufurahisha genge," anasema Wangwe.

Wangwe anafafanua kuwa mchakato wa kupata katiba ni jukumu la wananchi bila kujali itikadi za vyama vya siasa.

"Anatolea mfano wa mchakato wa kupata katiba kuwa mojawapo ule ulioendeshwa na Tume ya Jaji Warioba na kwamba ulivurugwa na wanasiasa wakati wa Bunge Maalum la Katiba. Labda nitoe wito kwamba, wanasiasa wahamasishe upatikanaji wa katiba mpya, lakini wasiingilie mchakato," anasema.

### TUSITARAJIE KITU

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Dk. Anna Henga, anasema kama kauli ya Chongolo ina ukweli, basi Watanzania wasitara-


INAENDELEA UK. 12

# Siasa zinavyokoleza migogoro ya ardhi Manispaa Kigamboni

## • Umma, mwekezaji watifuana kwa miaka 15

Na Faustine Feliciane

MOJA ya vitu vinavyokwamisha maendeleo katika maeneo mengi ni migogoro ya mara kwa mara baina ya pande mbalimbali, ambayo si kwamba inakwamisha maendeleo, lakini inaondoa amani na utulivu.

Mbaya zaidi, makosa yanafanyika pale migogoro hii hususani ile ya ardhi inapoingizwa kwenye siasa na kuleta misuguano hasa kwenye utatuzi wake ambao kila upande unavutia kwake ili kupata inachokusudia.

Hivi karibuni, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk Anjelina Mabula, anatoa msimamo wa serikali wa kuamua kuvalia njuga suala la migogoro ya ardhi na kuimaliza na kuweka mazingira ya kutoiruhusu kujirudia.

Kabla ya hapo, Dk. Mabula alishawahi kunukuliwa akieleza kuwa migogoro ya ardhi imekuwa ikichangiwa na viongozi na watendaji wa vijiji, mitaa na hata manispaa.

Kwa Dar es Salaam, hali ya migogoro ya ardhi imekuwa kilio kwa wananchi na wakazi wa maeneo mengi huku viongozi wa manispaa wakilalamikiwa kuwa sehemu ya tatizo hilo.

Kwa mfano Manispaa ya Kigamboni ni moja ya sehemu yenye migogoro mingi ya ardhi ambayo inahusisha wananchi kwa wananchi na wawekezaji dhidi ya wananchi upande mwingine.

Migogoro hiyo inatokana na ukweli kuwa eneo la Kigamboni lina mvuto kwa wawekezaji hasa kutokana na uwepo wa fukwe za bahari na hivyo kuwavutia zaidi wenye nia ya kuendeleza utalii, ambao wamenunua maeneo kwa shughuli hizo.

Moja ya migogoro inayosumbua wakazi wa manispaa hiyo ni mgogoro wa kugombea eneo la barabara kati ya wananchi na wawekezaji wa kata ya Kimbiji.

Wakazi wa eneo hilo wanamlalamikia mmoja ya wawekezaji katika eneo la Mikenge ambaye amejenga ukuta na kuzuia barabara inayotoka barabara kuu ya Kigamboni - Buyuni kwenda kwenye fukwe baharini.

Mwekezaji huyo anadaiwa kufunga barabara kwa madai kuwa maeneo hayo ni viwanja pacha vinavyoangaliana hivyo kufunga ni mchakato wa kuendeleza ardhi yake.



Halima Bulembo, Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni. **PICHA: MTANDAO**

> Mgogoro huo tayari ulikuwa umeshamalizwa kwa njia ya mazungumzo na makubaliano yalitangazwa kwenye mkutano wa wananchi wa Desemba 8, 2022.

### SIASA INAWAUMIZA

Mbwana Mwinyipingu ni mkazi wa eneo hilo aliyeishi zaidi ya miaka 40, anasema barabara hiyo inayolalamikiwa ilianzishwa takribani miaka 40 sasa na Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC) waliyoijenga ili kuwawezesha wafanyakazi kufika maeneo ya ufukweni kufanya utafiti wa gesi na mafuta.

Anasema kinachoendelea sasa ni maamuzi ya kisiasa yanayoingia kwenye utatuzi wa mgogoro huo uliodumu kwa zaidi ya miaka 15.

"Mimi nilifanya kazi kwenye mradi wa kuijenga, nilikuwa na vijana wenzangu wakati huo, tunasomba mawe kwa ajili ya ujenzi, na hata ilipokamilika ilitusaidia wananchi na wakazi wa maeneo haya, huyu bwana mkubwa mwekezaji anayelalamikiwa leo amemilikishwa hii barabara na imefungwa kwa kujengwa ukuta mkubwa tunashangaa imekuwaje?" anahoji Mwinyipingu.

Kauli hiyo inaungwa mkono na Mwenyekiti wa Kijiji cha Mikenge, Lameck Mayala, aliyekwenda mbali na kusema wananchi wanaona uongozi wa manispaa hiyo wanachochea mgogoro huo ambao tayari ulishaamuliwa na aliyekuwa Mkuu Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, aliyehamishiwa Mwanza.

"Kinachotushangaza kwa sasa, kwa nini maamuzi yale ya Mkuu wa Mkoa yamebatilishwa wakati tayari tunafahamu mchakato wa kulichukua eneo hili lenye mgogoro na kumlipa fidia huyu mwekezaji ulishaanza," anahoji Mayala.

"Ni kwani nini maamuzi ya viongozi wetu hawa yanapishana? Mkuu wa Wilaya mpya kaja kuamua vingine, nini kinaendelea, huu mgogoro hauhitaji maamuzi ya kisiasa," anasisitiza Mayala.

Uongozi wa Wilaya ya Kigamboni umetoa maamuzi mapya ya mgogoro huo ambapo yamepangwa kutekelezwa ndani ya miezi mitatu kuanzia sasa.

Akizungumza kwenye mkutano wa wazi na wananchi wa Mikenge, Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni, Halima Bulembo, anakubaliana na kutafuta barabara mbadala na kuachana na eneo hilo la mwekezaji.

"Naomba ndugu zangu wananchi tukubaliane na maamuzi haya tuliyoyafikia, barabara itajengwa eneo jingine na wataalamu wetu wameanza mchakato, tulitaka tuwafahamishe haya tuliyoafikiana," anasema Halima.

Anasisitiza makubaliano hayo waliyoyatoa ndiyo ya mwisho na kwa sasa wanaanza utekelezaji wake, uamuzi huo wa Mkuu wa Wilaya, unaibua malalamiko miongoni mwa wananchi ambao wamehoji kwa nini maelekezo ya ukuta huo kuvunjwa yamepuuzwa na kuletwa maamuzi mapya?

"Kwa nini Mkuu wa Mkoa Makalla ambaye tunafahamu utekelezaji wa makubaliano ulishaanza, barua zilishaandikwa kwenda kwa Kamishna Mkuu Ardhi Dodoma kuhusu maamuzi ya kutaka kuchukua eneo lenye mgogoro na kumlipa fidia mwekezaji ili kuruhusu barabara hiyo kufunguliwa yamekataliwa?" Anasema Arif Sheikh.

Ni mmoja wa wawekezaji kwenye maeneo ya fukwe ambaye ukuta huo uliojengwa umemzuia kufika kwenye eneo lake.

"Walikuja hapa wataalamu wakapita kwenye hizi njia ambazo leo wanasema ndizo watajenga, wataalamu mbele ya Mkuu wa Mkoa walikubaliana kuwa haiwezekani kujenga barabara mpya kutokana na korongo kubwa lililopo karibu na fukwe na ndiyo sababu walitoa maamuzi ya kurudisha hii ya zamani," anasema Arif.

Anaongezea:"Sasa wakati tunafuatilia na tukiamini mgogoro umemalizwa leo wanakuja na maamuzi mapya, tena mbaya zaidi wanataka kupitisha barabara eneo lile lile ambalo wataalamu waliona haiwezekani kuwepo kwa barabara kwa sababu ya lile korongo na maeneo mengi ya watu, haya maamuzi yametoka wapi na yapo kwa masilahi ya nani?"

Anasema mgogoro huo tayari ulikuwa umeshamalizwa kwa njia ya mazungumzo na makubaliano yalitangazwa kwenye mkutano wa wananchi wa Desemba 8, 2022.

Mkazi mwingine wa eneo hilo, Samuel John, anamwomba Rais Samia Suluhu Hassan, kuingilia shida hiyo ili haki ipatikane, baada ya mkwaruzano wa zaidi ya miaka 15.

# Chongolo aamsha mapya, huenda yajayo yakasikitisha

INATOKA UK. 11

"Kwa kauli ile, nina mashaka kama kàtiba mpya itapatikana. Kwa kweli amenifanya nibaki nikishangaa muda wote, anasema Dk. Anna.

Anasema mchakato wa kupata katiba mpya ni muhimu uendeshwe na watu huru wasio wanachama wa vyama vya siasa.

"Wanasiasa ndio waliotuangusha mwaka 2014 wakati wa Bunge Maalum la Katiba, kutokana na kila mwanasiasa kuvutia upande wake. Vyama vya siasa vinaweza kuweka wawakilishi wachache wa kushiriki maandalizi ya kupata katiba hiyo. Lakini si kubeba jukumu."

"Wakiwa wengi watatuletea katiba ya vyama yenye msilahi ya vyama vyao, si katiba ya wananchi, hivyo ni vyema wasiingilie mchakato huo," anasema.

Itakumbukwa kuwa Juni mosi mwaka huu, akiwa katika ziara ya kukagua utekelezaji wa Ilani ya CCM mkoani Iringa, Chongolo alitoa msimamo huo.

Anasema: "Watu wanapigapiga kelele huko ngoja niwaambie, CCM ndicho chama kiongozi, na ndicho kitakachoongoza mchakato wa katiba ya kisasa, iliyoandaliwa kisasa, itatengenezwa kupitia mikono, uongozi, usimamizi na uratibu wa CCM na si vinginevyo."

Aidha, akawataka watu wasidanganyike, kwa maelezo kwamba, wengi wanataka katiba kwa maslahi binafsi, hawazungumzii pembejeo za kilimo, usalama wa Watanzania wala miundombinu ya barabara.

UTAWALA BORA KATIKA JINSIA

# Dk. Samia akiwekeza kumwinua mama kila kona zinazoamua nchini

• Kuanzia Wizara, mikoani, mahakama, hadi taasisi

**Na Mwandishi Wetu**



Rosemary Senyamule, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma. **PICHA ZOTE: MTANDAO**



Mkurugenzi wa Bodi ya Maktaba Tanzania, Dk. Mboni Ruzegea.

NI katika hotuba zake za awali, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akaweka wazi nafasi ya mwanamke katika kuendesha na kusimamia nchi, akiitetea na kuanika azma kwa kaulimbiu 'kazi iendelee.'

Kimsingi, ni uendelezaji hatua kubwa za mageuzi ya kumtetea mwanamama nchini, hasa ikiangaliwa zaidi muundo wa kiserikali unaoboreshwa zaidi katika nafasi za jinsia na utawala bora nchini, hasa tangu zama za awamu ya tatu ya utawala nchini iliyoanza mwaka 1995.

Kuanzia awamu hiyo yenye nyenzo rasmi za -wizara na jinsia zikianzishwa, kisha ikaendelezwa kila awamu ikawa na maboresho yake, mfano katika awamu ya nne ya uongozi nchi.

Ni zama hiyo kwenye sura ya bajeti ngazi ya halmashauri zote kitaifa, kukabuniwa kutengwa fungu maalum kisheria za kukopesha vijana na kinamama kwa ajili ya miradi ya maendeleo yao.

Wakati kulipotokea kifo cha Rais Dk. John Magufuli, Rais wa Awamu ya Tano, kukalazimika mabadiliko kikatiba, makamu wake, Dk. Samia, akakasimiwa kisheria nafasi hiyo ya urais.

Ni hali iliyoleta tafsiri mpya si kitaifa pekee, bali ngazi ya kimataifa kwa kuwapo rais wa kwanza mwanamke Afrika Mashariki, Rais Samia, katika safari mpya baada ya majonzi, akianika uhalisia mwanzo kwa kauli, pia utashi na ndani ya muda mfupi vitendo, akionyesha 'haki na usawa jinsia' kwa vitendo.

Ushuhuda halisi ukachukua nafasi, pale Rais Dk. Samia akimteuua Mkurugenzi wa Mawasiliano Ikulu, Zuhura Yunus, kufanya ofisi hiyo ikahudumiwa na mwanamama hadi sasa na miezi mitatu na hata baadaye katika sura pana kiserikali, ikionyeshwa wazi nafasi ya kinamama nchini.

Kutimu wastani wa miezi mitatu, Rais Dk. Samia akafafanua uteuzi wake kwa vitendo, akiteua makatibu tawala wapya, asilimia 46 ya ni wanawake, huku akiwaachia changamoto waonyeshe tofauti katika utendaji katika nafasi wanazoenda kutumika, akiwaelekeza wawe watiifu kwa wananchi katika vituo vyao vya kazi na si kutofautiana.

Dk. Samia anaendelea: "Kati ya makatibu tawala 26, wanawake ni 12. Upande wa mahakama, niliteua majaji 28 ambao 13 ni wanawake na kufanya majaji wanawake kufika 40. Wabunge wanawake walikuwa 127 sasa 143 na nimeteua Katibu wa Bunge mwanamke, tunakwenda kufikia usawa wa kijinsia."

Ni aina ya uteuzi na usimamizi kitaifa wa rais huyo, akitumia mtindo wa kuwatambua kinamama wenzake, uwezo na nafasi zao, huku akiwawajibisha kwa vitendo tija inayotarajiwa ishuhudiwe kazini kwao.

Ni katika zama hizo, pia kukawapo kinamama katika uteuzi wa ukuu wa mkoa inayomjumuisha shujaa kazini, Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Mwanamvua Mrindoko.

> "Ni aina ya uteuzi na usimamizi kitaifa wa rais huyo, akitumia mtindo wa kuwatambua kinamama wenzake, uwezo na nafasi zao, huku akiwawajibisha kwa vitendo tija inayotarajiwa ishuhudiwe kazini kwao.

Mama huyo naye akiwa kazini akajibu wito wa uteuzi katika 'kazi iendelee' kwa kuchukua hatua kuwatetea kinamama wa Katavi, katika wajibu wake anajumuosja suala la kumlinda mama na haki ya kjinsia.

Hapo Mkuu wa Mkoa Mrindoko, anachukua hatua dhidi ya madhila kwa mama, akiwa ni jicho la Rais Dk. Samia, anapopiga marufuku adhabu kwa wajawazito kubebeshwa matofali na kuamriwa kuchimba mashimo katika baadhi ya zahanati na hospitali, wanaposhindwa kuhudhuria kliniki inavyotakiwa.

Ilielezwa kwamba, baadhi ya watumishi wa afya wamekuwa wakitoa adhabu hizo kwa kushirikiana na serikali za vijiji, ambazo huwasaka waliojifungua majumbani na kuwapa adhabu, wakiamini itaongeza idadi ya wanaohudhuria kliniki wakiacha kujifungua majumbani, katika jitihada za kupunguza vifo vya kinamama na watoto.

Mrindoko anatamka katika ujumbe unaofungamana na utashi wa Rais Dk. Samia kuhusu haki za kijinsia, kwamba: "Mkafikirie vizuri kitu gani mnaweza kufanya ili kuhamasisha wanawake na kinababa wawahi kliniki na wakajifungulie sehemu ya kutolea huduma za afya na sio kujifungulia nyumbani,"

### WALIVYO WAKURUGENZI

Kwa ngazi ya uongozi wa halmashauri nchini, wakati, mteule Rais Dk. Samia, akasawazisha uongozi wa baadhi ya wakurugenzi nchini mnamo Agosti Mosi, 2021 ikijumusha wateule wapya 69 na kati yao wakawapo kinamama 33, sawa na asilimia 48 na wanaume 36, sawa na asilimia 52.

Kwa mujibu wa taarifa ya Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), kulikuwapo wateule 15 waliojaza nafasi zilizokuwa wazi na 54 wamechukua nafasi za waliotenguliwa, hata kufikisha jumla ya wakurugenzi wanawake kuwa 55, sawa na asilimia 29 ya wakurugenzi wote 184 wa halmashauri za serikali za mitaa nchini.

"Uteuzi huu umefanya idadi ya viongozi wanawake aliowateua Rais Samia Suluhu Hassan tangu aapishwe rasmi Machi 19, 2021 kuwa Rais wa awamu ya sita katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufikia 144, sawa na asilimia 31% na wanaume kufikia 317 sawa na 69% ya wateuliwa wote 461," inatamka Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), katika taarifa yake Agosti, mwaka juzi.

"TGNP kama taasisi kinara katika kutetea Haki za Wanawake, ikiwamo kupigania ongezeko la idadi ya wanawake kwenye nafasi za uongozi katika vyombo mbalimbali vya uamuzi, tunapongeza jitihada hizi za makusudi zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita," inafafanua TGNP.

Pia ikatoa kauli kuwasihi waliopewa dhamana katika nafasi, kutambua hatima ya Watanzania, hususan wanawake ambao wengi hawako katika ajira rasmi, wana mitaji midogo na hawana ujuzi stahiki wa kufaidika na rasilimali za nchi kama vile madini, mafuta na gesi, ziko mikononi mwa maamuzi yanayofanywa na viongozi hao.

### ANAVYOSONGA NAO

Mwaka mmoja baadaye, Agosti, 2022, Dk. Samia akiingia katika mwaka wa pili wa uongozi wake, mbali na uhamisho wa kawaida wa wakuu wa mikoa 10, akawapo wakuu wa mikoa wapya tisa.

Ni katika safu hiyo mpya inayowajumuisha kinamama wawili; Halima Dendego, Mkuu wa Mkoa wa Iringa na Fatma Mwasa wa Morogoro, ambaye sasa amehamishiwa mkoa Kagera.

Januari mwaka huu, Rais akateua wakuu wapya wa wilaya 37, vilevile akawahamisha vituo vya kazi vya wakuu wa wilaya 48 na wengine 55 wakabaki kwenye vituo vyao.

Hapo nako kukaonekana kushamiri kipekee kinamama wachache ndio walioachwa, ikiendeleza mabadiliko makubwa kihistoria kwa fursa za kinamama katika uongozi.

Kwa sasa wakuu wa wilaya wapya, theluthi moja ni wanawake, ndani yao kuna vijana, pia wasomi kama Dk. Linda Peniel Salekwa, Mkuu wa Wilaya ya Mufindi.

Ni aina ya uteuzi kitaifa, unaosambaza uwakilishi wa kinanama kwa ngazi ya kitaifa, idadi yao ikiongezeka katika ngazi ya uamuzi, mfano kwa sasa Spika na Katibu wa Bunge ni mwanamke.

Pia, kuna idadi kubwa ya wabunge wanawake, majaji, mawaziri na wakuu wa kitaasisi, kama alivyo Mkuu wa Bodi ya Huduma za Maktaba, Dk. Mboni Rezegea, ambaye awali alikuwa nhadhiri wa Chuo Kikuu.

UASI WA WAGNER;

# Unavvyoleta mkanganyiko vita vya Russia, Ukraine

**Na Mwandishi Wetu**

• Yaelekea Putin inakula kwake, kisa? Kugeukana wao kwa wao



Kiongozi wa kundi la Wagner, Yevgeny Prigozhin. **PICHA: MTANDAO**

UASI wa muda mfupi wa Mkuu wa Jeshi la mamluki la Wagner Yevgeny Prigozhin, unamweka Rais wa Russia Vladimir Putin na serikali yake njia panda, tena kwenye eneo ambalo hatima yake haijulikani.

Licha ya kwamba ni mgogoro ambao wanauepuka, kwa sasa ukweli ni kwamba nini kitakachotokea baadaye baina ya Russia, kundi la Wagner na Ukraine bado hakijajulikana.

"Hatuna chochote ambacho tunaweza kutegemea au kukiangalia ili kujua kitakachofuata baada ya uasi huu," kinasema kituo cha Al Jazeera.

Matukio hayo ya uasi yalianza Jumamosi iliyopita, yakionekana kumshangaza kila mtu isipokuwa kundi la mamluki wa Wagner lililokuwa na vita kali. Vikosi vya Wagner vilichukua udhibiti wa haraka wa Rostov moja ya miji mikubwa ya Urusi, lakini kilichoshangaza havikabiliwa na upinzani au vilipata vikwazo kidogo kutoka kwa vikosi vya usalama vya ndani na cha ajabu mamluki walichukua makao makuu ya jeshi la mkoa huo wa Rostov.

Wanajeshi hao mamluki waliendelea kusonga mbele wakiingia Moscow makao makuu ya nchi kabla ya bosi wao Prigozhin kuamuru askari wake warudi nyuma kilomita 200 kutoka mji mkuu.

Prigozhin alikubali kwenda uhamishoni nchini Belarus baada ya kufanya makubaliano na Rais wa nchi hiyo Alexander Lukashenko, ambaye ni mshirika wa Putin.

### USIRI MAKUBALIANO

Ukosefu wa uwazi kuhusu mpango wa Lukashenko ni jambo linalowaacha wengi vinywa wazi. Kremlin au Ikulu ya Urusi inatangaza hadharani vipengele vya mpango huo, ikiwa ni pamoja na makubaliano kwamba Mkuu wa Wagner Prigozhin ataruhusiwa kwenda uhamishoni Belarus bila kukabiliwa na mashtaka ya jinai.

Ofisi ya Lukashenko huko Belarus inasema makazi hayo yana dhamana ya usalama kwa wanajeshi wa Wagner, lakini maelezo ni machache na taarifa kidogo, yanachanganya inasema Al Jazeera.

Hatua hiyo ina maswali mengi ambayo hayajajibiwa kuhusu mpango huo unaodhaniwa kuwa wameufikia, lakini hata yale ambayo yamejibiwa hayana maana, inasema runinga hiyo.

Joana de Deus Pereira, mtafiti mkuu katika masuala ya Russia na Ulaya ' RUSI Europe, anaiambia Al Jazeera kwamba ni "muhimu kuwa waangalifu na kuchambua kwa kina taarifa zinazotoka Urusi katika wakati huu.

### PRIGOZHIN MASHAKANI

Rais wa Russia ni mara chache ukimkosoa utabaki salama. Ni hasa dhidi ya wakosoaji wengi wake wakuu, kama vile kiongozi wa upinzani Alexey Navalny. Huyu anadaiwa ilishia kaburini kwa kupewa sumu au kufa kitatanishi, hivyo hatima ya Prigozhin ni mashaka matupu.

> Watu wanaomwingilia Vladimir Putin huwa na rekodi ya kukumbwa na mambo mabaya, huangukia pabaya nje tena chini ya dirisha. Tumewaona wakiondolewa na kwa njia nyingi za kikatili sana.

"Watu wanaomwingilia Vladimir Putin huwa na rekodi ya kukumbwa na mambo mabaya, huangukia pabaya nje tena chini ya dirisha. Tumewaona wakiondolewa na kwa njia nyingi za kikatili sana, "Msomi na Mtafiti Colin Clarke, anaiambia Al Jazeera.

Jumamosi, katika hotuba yake ya televisheni, Putin anamshutumu Prigozhin na Wagner kwa "usaliti" na "uhaini" na akaelezea vitendo vyake kama "rafiki aliyeaminiwa kugeuka na kukusaliti akifanya hivyo kwa askari wetu na Warusi."

"Wale wote waliotayarisha uasi watapata adhabu isiyoepukika," Putin anasema, na kuongeza, "Vikosi vya jeshi na mashirika mengine ya serikali yamepokea maagizo muhimu kwa utekelezaji."

Kwa msimamo huo mpango wa Prigozhin kupata hifadhi Belarus haumhakikishii usalama wake. Pengine Putin hataepuka kulipiza kisasi na kumwadhibu Prigozhin ikiwa anafikiria kuwa hiyo ni muhimu na huenda lazima atafanya hivyo.

Putin pia anathibitisha kutokukubaliana kwa hali yoyote na ukosoaji wa "operesheni maalum" ya Urusi kuivamia Ukraine, na ametoa wito wa "kujitakasa" ili kuondoa nchi yake kutoka kwa yeyote anayehoji uvamizi huo.

Prigozhin akiwa na jeuri anahoji hadharani sababu ya uvamizi kamili wa Urusi dhidi ya Ukraine ulioanza Februari 24, 2022 ukielekea mwaka mmoja na nusu sasa.

Tangu kufikiwa kwa makubaliano ya Lukashenko, Putin na maofisa wakuu wa Urusi wamefunga midomo kuzungumzia mustakabali wa Prigozhin.

Viongozi wengine wanaomuunga mkono Putin, hata hivyo, wamejitokeza na kumkosoa kigogo wa Wagner hadharani, akiwamo Rais wa Venezuela Nicolas Maduro na kiongozi wa Chechnya Ramzan Kadyrov.

Baada ya kukubaliwa kuishi Belarus, wanajeshi wa Wagner wamekubaliwa kuwa hawatakabiliwa na mashtaka, kulingana na mpango huo, na Serikali ya Urusi imekiri kuwa haitawashtaki wapiganaji wa Wagner walioshiriki katika maasi hayo, huku wale ambao hawakujiunga nao walipewa kazi na Wizara ya Ulinzi.

Prigozhin amewaamuru wanajeshi wake warudi kwenye kambi zao huko Ukraine, ambapo walikuwa wakipigana wakishirikiana bega kwa bega na vikosi vya Urusi.

Jumamosi iliyopita, vyombo vya habari vya Urusi viliripoti kuwa wanajeshi wa Wagner waliangusha helikopta kadhaa na ndege ya mawasiliano ya kijeshi za Urusi. Wizara ya Ulinzi ya Urusi haijatoa tamko lolote kuhusu madai hayo.

Wakati Prigozhin anaweza kuwa uso wa kikundi cha Wagner, jeshi hilo la mamluki ni kazi ya serikali ya Putin iliyoundwa ili kuwa na uwezo wa kufanya kazi katika nchi kadhaa na kukwepa ukweli. Kwa hili inawezekana kitaendelea, ikiwezekana chini ya jina jipya hata baada ya Prigozhin, kuchafua hali ya hewa.

### WAZIRI MTANDAONI

Waziri wa Ulinzi wa Russia, Sergey Shoigu, ameonekana kwenye video baada ya uasi wa Wagner, kwa mara ya kwanza baada ya mkuu wa kundi hilo Prigozhin kumtaka ajiuzulu.

Video inayoonekana Jumatatu Shoigu anawatembelea wanajeshi wa Urusi nchini Ukraine, japo maswali yanaibuka haijulikani ni lini video hiyo ilirekodiwa, ikidawa kuwa ililenga kuonyesha hali ya utulivu baada ya mamluki wa Wagner kuasi na kuteka mji wa Rostov-on-Don, na kuandamana bila kupingwa na yeyote wakielekea Moscow.

Wapiganaji wa Prigozhin walisonga mbele mji mkuu wakisema ni kuondoa kile walichokiita uongozi wa kijeshi fisadi na usio na uwezo wa Urusi . Hata hivyo, makubaliano na Kremlin na Lukashenko wa Belarus yalimaliza operesheni, hiyo ambayo iliisihangaza Urusi na dunia.



# Milioni 78/- za makusanyo ya h/shauri hazijapelekwa benki

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

TATIZO la kukusanya fedha kwenye vyanzo vya mapato ya ndani na kutozipeleka benki limeendelea kujitokeza katika halmashauri za mkoa wa Singida na zaidi ya Sh. milioni 78 zilizokusanywa hivi karibuni hazijapelekwa benki.

Kutokana na hilo, wakurugenzi wa halmashauri wameagizwa kuhakikisha kila siku wanafuatilia kwa wakusanyaji mapato kama wamepeleka fedha benki.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, aliyasema hayo jana kwenye kikao cha utekelezaji wa miradi na ukusanyaji wa mapato.

Serukamba alifafanua kuwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida ni Sh.milioni 21, Ikungi Sh. milioni 17, Iramba Sh. milioni 17, Manispaa ya Singida Sh.milioni 15, Mkalama Sh.milioni nne, Itigi Sh. milioni 3.1 na Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni Sh. milioni 1.1 hazijapelekwa benki.

"Tunaposisitiza ukusanyaji wa mapato siyo kwa sababu yangu mimi RC au RAS fedha zinazokusanywa zinasaidia kwenye miradi ya maendeleo msilichukulie suala la mapato kama ni 'personal'(binafsi) chama chetu cha CCM kitaweza kupata kura kama tumetekeleza miradi vizuri," alisema.

Alisema kila halmashauri ihakikishe inaweka chanzo cha mapato ambacho ina uhakika itakusanya mapato badala ya hivi sasa baadhi ya makusanyo yameshuka kutokana na kuweka chanzo kama cha kuuza viwanja ambavyo imeshindikana kuviuza.

**Kutokana na hilo, wakurugenzi wa halmashauri wameagizwa kuhakikisha kila siku wanafuatilia kwa wakusanyaji mapato kama wamepeleka fedha benki.**

Aidha, Serukamba aliipongeza Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama ambayo ndio inayoongoza kwa ukusanyaji mzuri wa mapato baada ya kufikia asilimia 104 ikilinganishwa na halmashauri nyingine.

Halmashauri ya Manispaa ya Singida imeshika nafasi ya pili baada ya Mkalama ambapo makusanyo yamefikia asilimia 98 ikifuatiwa na Singida DC asilimia 91, Ikungi 89, Manyoni 82, Itigi asilimia 72 na ya mwisho ikiwa Iramba yenye asilimia 70.

## Chongolo awataka wafanyakazi viwanda kuwa waadilifu

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, amewataka wafanyakazi wa Kiwanda cha Mbolea cha Intracom kuwa waadilifu na kujiepusha na vitendo vinavyomkwaza mwekezaji wa kiwanda hicho.



Chongolo aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipokuwa akizungumza na wafanyakazi wa kiwanda hicho kilichoko katika Kata ya Nala jijini hapo.

Alisema kuwapo kwa kiwanda hicho ni fursa kwao hivyo kuna umuhimu wa kuwa waadilifu na waaminifu kwa kushirikiana na mwekezaji.

Aidha, aliitaka menejimenti ya kiwanda hicho kuwekeza kwenye utafiti wa udongo kwa kulinganisha na mbolea wanayozalisha ili iwe na tija.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Kiwanda cha Mbolea cha Intracom, Nduwimana Nazaire, alisema kuwa kitakuwa kikubwa kwa Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati kutokana na uwezo wa kuzalisha tani milioni moja kwa mwaka.

Alisema: "Ninaimani na serikali ya CCM, kwamba ina nia na nguvu na uwezo wa kuweza kutumia viwanda vya ndani katika mfumo wa ruzuku ya mbolea ili mkulima aweze kupata mbolea kwa urahisi ikiwa serikali mtaamua kuweka pesa ya ruzuku kwenye viwanda vya ndani na mkulima atapata mbolea kwa wakati na kwa bei nafuu na kuondoa kero za wakulima."



Rais mstaafu, Dk. Jakaya Mrisho Kikwete, akizungumza na baadhi ya wakuu wa taasisi za Wizara ya Maji, walipokutana jijini Dodoma juzi. Kushoto ni Waziri wa Maji, Jumaa Aweso na Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# 'Kupungua tozo za barabara kutashusha gharama za intaneti'

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MKURUGENZI wa Tume ya TEHAMA, Dk. Nkundwe Mwasaga, amesema hatua ya serikali kupunguza tozo ya kupitisha mitandao kwenye barabara ili kuwezesha wananchi kufikiwa na intaneti kutoka dola za Marekani 1,000 hadi 100 kwa kilometa moja, itapunguza gharama za intaneti nchini.

Mei 13, mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan, aliahidi kushughulikia tozo hiyo ambayo ilikuwa ikilalamikiwa na watoa huduma na kusababisha vifurushi kuwa ghali.

Akizungumza na Nipashe jana, Dk. Nkundwe alisema kilio hicho kimetatuliwa kupitia bajeti ya serikali ya mwaka wa fedha ujao 2023/24 ambayo imepitishwa na Bunge juzi.

Alisema tozo hiyo ilisababisha gharama za intaneti kuwa ghali kutokana na kasi ya matumizi ya intaneti iliyopo kwa sasa.

Akizungumzia kuhusu mwamko wa vijana wenye ubunifu, mkurugenzi huyo alisema sababu ya kuanzishwa kwa tume hiyo ni kuwasaidia Watanzania hasa vijana wenye ubunifu wa TEHAMA.

"Tume hii ina miaka nane tangu imeanzishwa na serikali, sera ya kwanza ya TEHAMA ilitengenezwa mwaka 2003 na baada ya miaka 10 ilifanyiwa tathmini imetekelezwa vipi? Na changamoto zipo vipi? Kuna vitu vikajionesha cha kwanza sera haikuwa na mwenyewe kila mmoja alikuwa anatekeleza kivyake," alisema.

Aliongeza: "Dhamira ya serikali ni kuhakikisha vijana wanapata fursa za ndani na nje ya nchi, mikopo na hili wakaona tukuze kupitia vijana tangu tumeanza tumeona vijana wana uwezo mkubwa wa kubuni na wanajituma."

Alisema tume hiyo inajukumu la kuratibu ubunifu wao na kuzitambua kwa kushirikiana na Ofisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA) na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA).

"Nitoe rai kwa vijana wenye ubunifu kuzisajili ili kuwa na uhakika kwamba hakuna atakayeuchukua ubunifu wako na kikubwa zaidi tumeona kuna watu wanatoka nje ya nchi wanakuja kununua ubunifu Tanzania.

Watu hawapendi kununua kitu ambacho hakijasajiliwa, kitu ambacho hakijasajiliwa mnunuzi anaweza kuhisi umemwibia mtu mwingine," alisema.

Alisema watu wenye ubunifu wa TEHAMA wafike kwenye tume hiyo ili kuwapa ushauri na kuwafungulia fursa za kunufaika na bunifu zao.

Alisema: "Watu ambao wana mitaji na wapo tayari kutoa ili ubunifu ukue wapo na wapo wengine Tanzania wameshakuja kuniona mimi, wapo wengi ila sasa ubunifu kuwa katika hatua ambayo mtu anaweza kuweka fedha yake inatakiwa vitu vingine vifanyike."

Aliongeza: "Kuna kitu nimekiona kwa wabunifu wengi wana uwezo mkubwa sana katika kufanya vitu kwenye eneo la kiufundi kama kutengeneza mfumo na vitu vingine wanajua lakini eneo ambalo tunahitaji kuwasaidia zaidi ni eneo la biashara."



# Wamiliki hoteli, 'gesti' waonywa kupandisha bei sikukuu Nanenane

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI mkoani Mbeya imewapiga marufuku wamiliki wa hoteli na nyumba za kulala wageni kupandisha bei za vyumba wakati wa maonyesho ya Sikukuu ya Wakulima (Nanenane) ambayo yanatarajiwa kufanyika mkoani humo kuanzia Julai 25 mpaka Agosti 8, mwaka huu.

Aidha, imewatahadharisha wamiliki wa vyombo vya usafiri wa umma hasa mabasi ya abiria watakaopandisha nauli ama kukatisha safari kuwa watachukuliwa hatua kali za kisheria ili kukomesha tabia hiyo.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alitoa tahadhari hiyo jana alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu maandalizi ya maonyesho hayo ambayo kwa mara ya kwanza yatakuwa ya kimataifa.

Alisema kuna kamati maalumu ambayo imeundwa kwa ajili ya kufuatilia hali ya hoteli katika mkoa huo kwa ajili ya kupokea wageni mbalimbali watakaoshiriki maonyesho hayo.

Alisema wameshatoa maelekezo kwa wamiliki wa hoteli kuhakikisha wanatoa mafunzo kwa wafanyakazi wao ili wawahudumie vizuri wageni watakaofika kwenye maeneo hayo.

"Vyombo vya ulinzi na usalama pia vitakuwapo kuhakikisha kwamba wageni wanaishi kwa amani na utulivu wakati wote wa maonyesho, lakini vitahakikisha vyombo vya usafiri vinafanya kazi kwa kuzingatia sheria," alisema Homera.

Katika hatua nyingine Homera alisema maonyesho hayo yatazinduliwa rasmi Agosti Mosi na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango na kuhitimishwa Agosti 8 na Rais Samia Suluhu Hassan.

Alisema mbali na viongozi hao wakuu wa nchi, pia kuna viongozi mbalimbali ambao watakuwa wanatembelea katika maonyesho hayo kwa siku zote za maonyesho na hivyo akawataka wananchi kujitokeza kwa wingi.

Alisema mpaka sasa zaidi ya mataifa 30 duniani kote yakiwamo ya ukanda wa SADC yamethibitisha kushiriki na wanaendelea kutoa mialiko kwa mataifa mbalimbali kwenda kushiriki.

"Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, ndiyo inayoalika mataifa mbalimbali kuja kushiriki maonyesho haya, lakini kuna mataifa mengi ambayo yameshathibitisha kushiriki," alisema Homera.

Aliyataja baadhi ya mataifa yaliyothibitisha kuwa ni pamoja na Malawi, Zambia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Msumbiji, Namibia na India.

Alisisitiza kuwa serikali inaendelea kualika mataifa mbalimbali kupitia mabalozi wanaofanya kazi nchini pamoja na nchi zingine za kidiplomasia.

Aliwataka wananchi wa mikoa yote ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kujitokeza kwa wingi kwenye maonyesho hayo ili kujifunza mbinu na teknolojia za kisasa za kilimo ambazo zitawasaidia kuongeza uzalishaji.

Katibu Tawala Msaidizi wa Uchumi na Uzalishaji, Said Madito, alisema maonyesho hayo yatakuwa na tija kwa wananchi wa mikoa hiyo pamoja na nchi nzima kutokana na teknolojia nyingi kuonyeshwa.

Alisema endapo wananchi watajitokeza kujifunza kuna uwezekano hata uzalishaji wa mazao mbalimbali ya chakula na biashara ukaongezeka na kuwa na uhakika wa chakula na kipato.



Meneja wa Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) Kanda ya Mashariki, Adonis Bitegeko, akizungumza katika mkutano wa wadau na wasambazaji wa vifaa tiba na viambatanishi wenye lengo la kutoa tathmini ya ufanisi wa mwaka 2023 jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# TBS yafanya operesheni kamata bidhaa 'feki' mikoa 3

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

VILAINISHI vya vyombo vya moto, nguo za ndani za mitumba na nyaya za umeme zisizokidhi viwango vya ubora vyenye thamani ya zaidi ya Sh. 5,000,000 vimekamatwa katika mikoa mbalimbali ya Kanda ya Magharibi.

Vitu hivyo vimekamatwa kufuatia operesheni maalum iliyoendeshwa na maofisa wa Shirika la Viwango nchini (TBS) Kanda ya Magharibi kwa kushirikiana na vyombo mbalimbali vya dola.

Operesheni hiyo maalumu ilifanyika katika mikoa ya Rukwa, Katavi na Kigoma ambapo wakaguzi wa shirika hilo walibaini uwepo wa bidhaa hizo zilizopigwa marufuku kutumika nchini zikiwa zinaendelea kuuzwa madukani.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kukamilika kwa operesheni hiyo, Ofisa wa TBS, Elisha Meshack, alisema operesheni hiyo ya ukaguzi imeenda sambamba na utoaji elimu kwa wenye maduka yanayouza bidhaa hizo ili waweze kuzingatia matakwa ya viwango na kufuata sheria na taratibu zilizowekwa.

"Operesheni hii ambayo imemalizika katika mikoa ya Rukwa, Katavu na Kigoma ni endelevu na lengo ni kuhakikisha soko la Tanzania linakua na bidhaa bora na salama kwa matumizi ya wananchi na mazingira," alisema Meshack.

Alitaja madhara ambayo mtu anaweza kuyapata kwa kuvaa nguo za ndani za mitumba zilizopigwa marufuku kuwa ni magonjwa ya ngozi pamoja na yale yanayoshambulia sehemu za siri.

Kwa madhara ya kutumia nyaya zilizopigwa marufuku, Meshack alisema ni kuunguliwa na vitu na hata kuweza kusababisha vifo.

Kuhusu madhara ya matumizi ya mafuta ya breki aina ya dot 3, Meshack alisema yanaweza kusababisha breki zikafeli na kusababisha ajali ambazo zinaweza kusababisha uharibifu wa mali na hata vifo.

Kwa upande wake Ofisa Masoko wa TBS, Deborah Haule, alisema kuwa mpaka sasa wamefanikiwa kukamata bidhaa zenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 25 katika operesheni hiyo na kusisitiza kuwa operesheni hiyo ni endelevu.

"Operesheni hii ni endelevu na tutaendelea na ukaguzi wa bidhaa hafifu sokoni mpaka pale tukapojiridhisha kuwa Tanzania yetu ni salama na wafanyabiashara wanasimamia ubora wa bidhaa katika maeneo yote," alisema Haule.

Haule alitoa wito kwa wafanyabiashara wote kufuata matakwa ya viwango wanaponunua na kutengeneza bidhaa ili kujiepusha na hasara wanazoweza kupata pale bidhaa zao zitakapogundulika kuwa zina ubora hafifu na vile vile aliwasisitiza kuwasiliana na ofisi za TBS pale wanapoona wana mashaka na bidhaa yoyote.

Kwa upande wao baadhi ya wafanyabiashara wameomba elimu hiyo izidi kutolewa na kudhibiti wafanyabiashara wakubwa wanaoingiza bidhaa ambazo zilipigwa marufuku.

Mmoja wa wafanyabiashara wa mkoani Kigoma, Ibrahim Ramadhani, alipongeza kazi nzuri inayofanywa na TBS na kushauri utaratibu huo uendelee ili soko la Tanzania liwe na bidha zinzokidhi matakwa ya ubora.

# Polisi yataja chanzo kifo cha bosi aliyefia hotelini

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya limesema Mkurugenzi wa Kampuni ya Giant Tanzania Printers Ltd ya jijini Dar es Salaam, Degratius Magubo ambaye alikutwa amefariki kwenye moja ya nyumba za kulala wageni jijini Mbeya alikuwa amekunywa pombe na dawa za binadamu.

Magubo alikutwa Juni 21, mwaka huu, akiwa amefariki ndani ya chumba alichokuwa amepanga kwenye moja ya nyumba za kulala wageni, huku chanzo cha kifo chake kikiwa hakifahamiki jambo ambalo lilizua wasiwasi.

Baada ya kifo cha mfanyabiashara huyo, baadhi ya taarifa zilianza kuzagaa kwenye mitandao ya kijamii zikieleza kuwa aliuawa huku zikiwa hazitaji mtu aliyemuua.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi, Benjamin Kuzaga, aliwaambia waandishi wa habari juzi kwamba baada ya kupokea taarifa za kifo hicho walituma timu ya makachero kwenda kufuatilia.

Alisema walifanya uchunguzi na kubaini kuwa kwenye chumba alichokuwa amelala mfanyabiashara huyo kulikuwa na pombe aina ya Grants na dawa za binadamu ambazo alikuwa anatumia.

Alisema waliwatumia wataalamu wa upasuaji kutoka katika Hospitali ya Kanda ya Rufani ya Mbeya kuufanyia uchunguzi mwili wa mfanyabiashara huyo.

"Mwili huo ulifanyiwa uchunguzi mbele ya wanafamilia ambao awali walitoa masharti kwamba mwili huo hautakiwi kufanyiwa uchunguzi bila wao kuwepo, kwa hiyo tulifanya uchunguzi na wao wakishuhudia," alisema Kuzaga.

Alisema baada ya kumaliza uchunguzi huo walichukua baadhi ya sampuli na kuzipeleka katika Ofisi ya Wakala wa Mkemia Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kufanya uchunguzi zaidi juu ya kifo hicho.

Alisema baada ya kupokea majibu ya uchunguzi huo kutoka kwenye maabara ya Mkemia Mkuu, watalinganisha na kile walichobaini wao kisha watatoa taarifa ya mwisho.

Kuzaga aliwataka wananchi kuacha kutoa taarifa za uongo kupitia mitandao ya kijamii kwa maelezo kuwa taarifa hizo zinasababisha taharuki kwa jamii.



## Wafanyabiashara wanaodanganya kuchukuliwa hatua

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, ameuagiza uongozi wa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kuwachukuia hatua stahiki wafanyabiashara wanaojihusisha na udanganyifu wa bidhaa kwa lengo la kujiongezea faida.

Aliyasema hayo wakati akizungumza katika kikao cha Baraza la Wawakilishi Chukwani Zanzibar.

Alisema lakini wapo baadhi ya wafanyabiashara wanaochakachua bidhaa hizo ikiwamo mchele aina ya Mbeya kuuchanganya na michele mengine isiyo na hadhi sawa hali ambayo inapoteza ladha na uhalisia wake.

Aidha, aliwataka wafanyabiashara wenye tabia hiyo kuacha mara moja na kuwa waadilifu katika kujitafutia riziki za halali pamoja na kuwapatia wananchi huduma bora isiyo na udanganyifu wa aina yoyote.

Makamu huyo alisema kuwa serikali imeipa kazi za uendeshaji wa Bandari ya Malindi Kampuni ya Africa Global Logistics (AGL) kwa lengo la kurahisisha ushushwaji wa mizigo ambapo kwa sasa meli inashusha mzigo ndani ya siku mbili tofauti na awali uliokuwa ukichukua wiki moja au zaidi.

Alisema serikali imebinafsisha baadhi ya huduma za vipimo katika Hospitali ya Rufani ya Mnazi Mmoja zikiwamo huduma za Ultrasound, CT- scan, maabara na MRI kwa lengo la kuhakikisha ufanisi na utoaji huduma bora za afya kwa wananchi.

**Aliyasema hayo wakati akizungumza katika kikao cha Baraza la Wawakilishi Chukwani Zanzibar.**

# CRDB yapongezwa kwa kukusanya Bil. 700/- za kukopesha wajasiriamali

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

SERIKALI imeipongeza Benki ya CRDB kwa kukusanya zaidi ya Sh. bilioni 700 za kuwakopesha wafanyabiashara wadogo na wa kati nchini katika maadhimisho ya Siku ya Wajasiriamali Duniani.

Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), Abdalla Hussein Kombo, aliyekuwa mgeni rasmi katika maadhimisho hayo jana alisema jitihada zinazofanywa na benki hiyo zinaonyesha dhamira ya dhati iliyonayo katika kuchochea ujasiriamali nchini.

"Takwimu zinaonyesha ni asilimia 96 ya biashara nchini ni biashara ndogo na za kati, ambapo watu milioni 24 wameajiriwa katika sekta hii. Hivyo, jitihada hizi zinazofanywa na Benki ya CRDB ni muhimu sana katika kuboresha sekta hii ambayo inatoa mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi wa Taifa letu," alisema Kombo.

Waziri Kombo alibainisha kuwa sekta ya ujasiriamali inachangia asilimia 33 katika Pato la Taifa, akifafanua kuwa katika kila Sh. 100, Sh. 33 ambazo ni sawa na theluthi moja, zinachangiwa na biashara ndogo.

Benki ya CRDB inatajwa kuwa kinara katika uwezeshaji wa wajasiriamali nchini huku mwaka huu ikitunukiwa tuzo ya Benki Bora kwa Uwezeshaji wa Wajasiriamali na jarida maarufu la Marekani la Global Finance.

Kwa Zanzibar, Waziri Kombo alisema serikali inajivunia ushirikiano na Benki ya CRDB kupitia programu ya 'Inuka na Uchumi wa Buluu' kuwainua wajasiriamaili ambapo Sh. bilioni 60 zimetengwa. Programu hiyo ambayo inatoa ufadhili wa mitaji kwa wajasiriamali bila riba, inatajwa kuwa moja ya programu bunifu zenye msukumo mkubwa wa kuwainua wajasiriamali nchini.

Ofisa Mkuu wa Biashara wa Benki ya CRDB, Boma Raballa, alisema wanatambua na kuthamini shughuli za kijasiriamali katika kusukuma gurudumu la maendeleo ya wananchi na Taifa kwa ujumla, jambo ambalo limeifanya benki hiyo kushirikiana na wadau mbalimbali ndani na nje ya nchi katika kuboresha sekta hiyo.

"Katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita wakati dunia ikishuhudia misukosuko ya kiuchumi iliyochangiwa na janga la UVIKO-19 na vita vya Ukraine, benki yetu kwa kushirikiana na washirika wa kimataifa ilikusanya zaidi ya Sh. bilioni 700 ambazo zinaendelea kusaidia biashara za wajasiriamali ambazo nyingi ziliathirika kwa kiasi kikubwa," alisema Raballa.

Raballa alisema wameshirikiana na wadau wa ndani na kimataifa likiwamo Shirika la Fedha la Ufaransa Proparco, Shirika la Fedha Kimataifa (IFC), Mashirika ya Marekani ya Maendeleo ya Kimataifa (USAID) na DFC, Benki ya Uwekezaji ya Umoja wa Ulaya, Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB) na Mfuko wa Dhamana Afrika (AGF) kukusanya kiasi hicho cha fedha.

Raballa alisema ili sekta ya ujasiriamali itoe mchango wake kikamilifu katika kukuza uchumi wa Taifa, kunahitajika huduma na mifumo shirikishi itakayowasaidia wajasiriamali kufanikisha malengo yao.

Kwa kutambua hilo, alsiema Benki ya CRDB ilikuwa benki ya kwanza nchini kuanzisha huduma kwa ajili ya wajasiriamali mwaka 2005 ambapo tangu kipindi hicho imekuwa inawekeza kwa kiasi kikubwa katika bidhaa na huduma bunifu za wajasiriamli.

Huduma na bidhaa hizo zinajumuisha akaunti maalum ya Hodari ambayo ni mahsusi kwa ajili ya wajasiriamali, mifumo ya kidijitali ya usimamizi wa biashara, mafunzo ya ujasiriamali ndani na nje ya nchi, na kutoa mikopo ya mtaji kwa wajasiriamali walio katika sekta tofauti za uchumi.

"Ninajivunia kuwajulisha kuwa kupitia jitihada hizi, benki yetu imekuwa kinara katika kuwawezesha wajasiriamali kwani hadi Mei 2023 tulikuwa tumetoa mikopo yenye thamani ya zaidi ya Sh. trilioni 3.4 kwa wajasiriamali zaidi ya 200,000 na wengine zaidi ya 50,000 wakinufaika kwa mafunzo tuliyoyatoa," alisema Raballa.

Raballa alisema hivi karibuni Benki ya CRDB kupitia Taasisi yake ya CRDB Bank Foundation imeendelea kupanua wigo wa kuwainua wajasiriamali wadogo kupitia programu endelevu ya 'Imbeju' inayolenga kufanya uwezeshaji wa biashara changa na wajasiriamali vijana na wanawake kupitia mafunzo, ushauri, na mitaji wezeshi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Chama cha Wanawake Wafanyabiashara Tanzania (TWCC), Mwajuma Hamza, aliipongeza Benki ya CRDB kwa kuwa mdau mkubwa wa sekta ya ujasiriamali hususan kwa kuweka mbele uwezeshaji wa wajasiriamali wanawake kupitia CRDB Malkia inayojumuisha Akaunti ya Malkia na mikopo maalum ya kinamama ijulikanayo kama WAFI (Women Access to Finance Initiatives).




Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Elimu kwa Umma wa Mamlaka ya Masoko na Mitaji ya Dhamana (CMSA), Charles Shirima, akizungumza na waandishi wa habari baada ya ufunguzi wa mafunzo kwa wajasiriamali Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Upatikanaji mitaji wajasiriamali Zanzibar tatizo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKURUGENZI Mkuu wa Wakala wa Maendeleo wa Viwanda Vidogo na Kati Zanzibar (SMIZDA), Soud Said Ali, amesema kuna changamoto ya upatikanaji wa mitaji kwa wajasiriamali visiwani humo.

Amesema hali hiyo inasababishwa na wengi wao kutokuwa na sifa za kupata mitaji katika taasisi za kifedha.

Aliyasema hayo juzi visiwani Zanzibar wakati akifungua mafunzo kwa wajasiriamali kuhusu njia mbadala ya kupata mtaji kwa shughuli za maendeleo, iliyoandaliwa na Mamlaka ya Masoko na Mitaji ya Zamana Tanzania (CMSA).

Alisema katika taasisi za kifedha wanahitaji mambo mbalimbali ikiwamo vitu vya thamani wanavyomiliki ili kupatiwa mitaji kupitia benki lakini hushindwa kutokana na kutokua na sifa hizo.

Alisema kupitia mafunzo hayo watapata elimu jinsi ya kupata fedha za kuendeleza biashara zao.

Aidha, alisema wajasiriamali wanachangamoto za upatikanaji wa masoko, mashine kwa ajili ya uzalishaji, mashine kwa ajili ya vifungashio na maeneo ya uzalishaji, hivyo mafunzo hayo ni fursa nzuri kwao.

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano cha Elimu kwa Umma wa CMSA, Charles Shirima, alisema lengo la kufika Zanzibar ni kutoa elimu kwa wajasiriamali wa Zanzibar kutambua jukwaa la mitaji halaiki ili kuwekeza katika biashara zao.

Alisema unapochangia mtaji kwa ajili ya biashara unapata fursa ya kuwekeza kifedha na kuchangia ukuaji wa uchumi.

Alisema biashara ndogo hazina sifa za kupata mikopo katika taasisi za kifedha, hivyo wanaziwezesha biashara hizo kupata mitaji kupitia majukwaa ya halaiki.

Aidha, alisema wameandaa kanuni na miongozo ya kushiriki katika mifumo wa halaiki na miongozo hiyo itachapishwa katika gazeti la serikali.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JANUARY MAYENGO YEYERE** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T.510 AAT.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.

TAARIFA YA POLISI

**MBE/MBE/RB/218176/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

BENITHO BATHOLOMEO MBWILO anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba ya usajili T 495 CVD – TOYOTA ESCUDO. Chassis namba TL52W100778. Engine namba J20A0986521. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Taarifa ya polisi:

NJO/MAK/RB/208355/2023.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**STEPHEN MICHAEL** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0156-0141** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **TANGA SECONDARY SCHOOL** mwaka **2000.** Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA:**

**DAR/MSI/RB/181762/2023**

## KUPOTEA KWA CHETI



**DOMINICK PAULO SHAIDI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0395-0047** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **BOZA SECONDARY SCHOOL** mwaka **1987.** Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: DAR/CEN/RB/216583/2**023

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA, KANDA YA BUKOBA**
**MAOMBI MADOGO YA ARDHI NA. 14/2022**
**THEOPISTA GERVAZ ...............MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**MAGRETH AGRICOLA RWIZA............MJIBU MAOMBI**

**WITO/ KUITWA SHAURINI**

**Kwa: MAGRETH AGRICOLA RWIZA Popote Ulipo**

Hii ni kukutaarifu kwamba shauri la Maombi tajwa juu imepangwa kusikilizwa tarehe 30 mwezi Juni mwaka 2023 saa 3:00 asubuhi, mbele ya Mh. A.Y. MWENDA Jaji wa Mahakama Kuu Kanda ya Bukoba. Kwa hiyo unapaswa kuhudhuria wewe mwenyewe au mwakilishi wako anayeruhusiwa kisheria. Endapo hautahudhuria wewe mwenyewe au mwakilishi wako shauri hili litasikilizwa bila wewe kuwepo.

Imetolewa kwa mkono wangu na chapa ya Mahakama leo hii tarehe 26 mwezi Juni mwaka 2023.

NAIBU MSAJILI

MAHAKAMA KUU YA TANZANIA

BUKOBA

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**PETER RAPHAEL MWARIA** wa Majengo Kahama, Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T. 720 AUM** aina ya **RAV 4.** Yeyeote atakayeiona ataoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake.

Taarifa ya polisi.

**KAH/RB/445/2023.**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**Probate and Administration Cause No. 50 of 2023**
**In the matter of the Estate of the late**
**VIANEY ABDON MLAY of CHAMWINO**
**within Dodoma Region**
**And**
**In the matter of the application for letters of administration by**
**GODLOVE ELIAKANA NKOLIALA**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 163)**

All PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the **26 Day of JUNE , 2023**

**Date at Dodoma this 8 day of MAY , 2023.**

RESIDENT MAGISTRATE DODOMA DISTRICT

RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BENEDICT VALENTINE LYARUU**

anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili namba **T601 CVM .** kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA:**

**DAR/URA/RB/216342/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FLORENCE PATRICK KASSERA**

anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili namba **T482 DCL .** kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:

**DAR/URA/RB/216342/2023**

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 17 OF 2023**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE DANIEL YOHANA MNKANDE**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LATER OF ADMINISTRATION**
**BY DOROTHEA DANIEL MNKANDE**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of probate Rules GN 369 OF 1963)**

ALL PERSON claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.

Objections to the grant should be field on or before the 24 day of July 2023.

**Dated at Korogwe this 21 day of June 2023**


# OFISI ZA MATANGAZO
# MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
# PO.BOX 31042,
# DAR ES SALAAM.
# MOB: +255 - 0677020701
## E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ,
## WEBSITE: WWW.IPPMEDIA.COM



**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

MAKALA KIMATAIFA

# Putin: Viongozi wa uasi Wagner watachukuliwa hatua kisheria



Kiongozi wa kikundi cha mamluki cha Wagner, Yevgeny Prigozhin. **PICHA ZOTE: MTANDAO**



Rais wa Russia, Vladimir Putin.

**MOSCOW,** Russia

RAIS wa Russia, Vladimir Putin, amewashutumu viongozi wa uasi wa Wagner kwa kutaka kuiona Russia ikizongwa na mapigano ya umwagaji damu, huku akiapa kuwachukulia hatua za kisheria waandalizi wa uasi huo.

Wagner ni jeshi la kibinafsi la mamluki ambalo limekuwa likipigana pamoja na jeshi la kawaida la Russia nchini Ukraine.

Rais Putin anayasema hayo kupitia video iliyotolewa jana, licha ya kwamba hakumtaja moja kwa moja kiongozi wa Wagner Yevgeny Prigozhin, ambaye awali alikana kujaribu kuupindua utawala wa Putin.

Pia Rais Putin anawaita wanajeshi wa kawaida wa Wagner wazalendo ambao wangeruhusiwa kujiunga na jeshi, kwenda Belarusi au kurudi nyumbani.

Prigozhin anadai kuwa uasi wa muda mfupi wa Wagner kuteka mji mkubwa wa Russia kabla ya kuelekea Moscow katika safu ya magari ya kijeshi, ulikuwa jibu kwa mipango ya serikali ya kuchukua udhibiti wa moja kwa moja wa Wagner.

Inaelezwa kuwa mwezi huu Russia ilisema makundi ya kujitolea yangeombwa kutia saini mikataba ya Wizara ya Ulinzi katika hatua inayoonekana kuwa tishio kwa Prigozhin kudhibiti kundi la Wagner.

Mkuu huyo wa mamluki anasema uasi wake pia ulikuwa maandamano dhidi ya makosa yaliyofanywa na maofisa wa ulinzi wakati wa vita na Ukraine, akisisitiza kwamba Wagner anachukua hatua kila wakati kwa masilahi ya Russia tu.

Inaelezwa kuwa hayo yalikuwa maoni ya kwanza ya umma kwa Prigozhin tangu kukubali makubaliano ya kusitisha uasi, ambayo inaripotiwa kuwa ni pamoja na yeye kwenda Belarus na mashtaka yote ya jinai dhidi yake yakitupiliwa mbali, ingawa vyombo vya habari vya serikali ya Russia, vikiwanukuu maofisa, vimeripoti kuwa bado anachunguzwa.

Prigozhin anasema alimaliza maasi kuepusha kumwaga damu ya wanajeshi wa Russia, na kwamba baadhi ya raia wa taifa hilo walisikitishwa na maandamano yaliyotokea, huku akisisitiza kuwa hakuwa na nia ya kujaribu kupindua mamlaka iliyochaguliwa ya Russia.

Aidha, inabainishwa kuwa hadi sasa Prigozhin hajulikani wapi alipo na nini atafanya baadaye.

Katika hotuba yake fupi kwa watu wa Russia, Rais Putin anasema waandalizi wa maandamano ya Moscow watafikishwa mbele ya sheria, akieleza kuwa mshirika wake wa zamani Prigozhin aliisaliti Russia.

Hata hivyo, Putin anatumia hotuba hiyo kama jaribio la kuthibitisha mamlaka yake, na kupinga maoni yaliyopo kwamba majibu yake kwa uasi wa Wagner yalikuwa dhaifu, ikielezwa kuwa sauti yake katika hotuba hiyo fupi, iliyorekodiwa ilikuwa ya hasira huku midomo yake ikijikunja.

> **Nawashukuru wale wanajeshi na makamanda wa kikundi cha Wagner ambao walifanya uamuzi sahihi pekee hawakugeukia umwagaji damu wa kindugu, walisimama kwenye mstari wa mwisho.**

**WALISALITI NCHI**

Ujumbe wa Rais Putin ulieleza kwamba wale walioandaa uasi walikuwa wameisaliti nchi yao na watu wao na walikuwa wakifanya kazi ya maadui wote wa Russia kwa kujaribu kuiingiza katika umwagaji damu na mgawanyiko.

Vile vile, anazishutumu nchi za Magharibi kwa kutaka Warussia wauane, lakini Rais wa Marekani, Joe Biden aliuambia mkutano na waandishi wa habari Jumatatu kwamba Marekani na washirika wake hawakuhusika katika uasi wa Wagner ambao haukufaulu.

Rais Putin, anasema kuwa usimamizi wake wa mgogoro huo umeepusha maafa.

Pia anasema atatimiza ahadi yake ya kuruhusu wanajeshi wa Wagner ambao hawakutaka umwagaji damu kwa ndugu zao kutokea, kuondoka kuelekea Belarus.

"Nawashukuru wale wanajeshi na makamanda wa kikundi cha Wagner ambao walifanya uamuzi sahihi pekee hawakugeukia umwagaji damu wa kindugu, walisimama kwenye mstari wa mwisho," amesema.

"Leo, una fursa ya kuendelea na huduma yako kwa Russia kwa kutia saini mkataba na Wizara ya Ulinzi au vyombo vingine vya kijeshi na kutekeleza sheria, au kurudi kwa familia yako na watu wa karibu, wale wanaotaka wanaweza kuondoka kwenda Belarus, ahadi ambayo nilitoa, itatekelezwa," amesema Putin.



Rais wa Belarus Alexander Lukashenko

Putin anasema "hatua zilichukuliwa ili kuepusha umwagaji damu mwingi, mwanzoni mwa uasi huo na kwamba waandalizi wake waligundua kuwa vitendo vyao ni vya uhalifu".

**AMPONGEZA LUKASHENKO**

Kiongozi huyo pia anapongeza umoja wa jamii ya Russia na kumshukuru kiongozi wa Belarus Alexander Lukashenko, ambaye inasemekana ndiye aliyefanikisha mpango huo wa kumaliza maasi, kwa juhudi zake za kutatua hali hiyo kwa amani.

Mazungumzo ya Rais Putin kuhusu nchi iliyoungana nyuma yake yanatofautiana vikali na picha za Jumamosi kutoka mji wa kusini wa Rostov, ambao kundi la Wagner lilikuwa limedhibiti na kwamba wenyeji waliwapigia makofi wapiganaji mitaani, wakiwakumbatia na kupiga nao picha.

Inaelezwa kuwa labda hiyo ndiyo sababu Putin aliwapa wanachama wa Wagner njia ya kutoka, akipendekeza kuwa wamedanganywa na kutumiwa.

Uasi wa wiki iliyopita ulifuatia miezi kadhaa ya mvutano uliokua kati ya Wagner na uongozi wa kijeshi wa Russia.

Mapigano yaliibuka Ijumaa usiku wakati mamluki wa Wagner walipovuka mpaka kutoka kambi zao huko Ukraine na kuingia katika mji wa kusini wa Rostov-on-Don eneo la vita vya Russia vinaelekezwa kutoka.

Kisha waliripotiwa kuchukua kamandi ya jeshi la mkoa huku safu ya magari ya kijeshi ikienda kaskazini kuelekea Moscow.

Prigozhin anadai maandamano yake ya haki yalifichua matatizo makubwa ya usalama kote nchini humo.

Pia anataja jukumu ambalo Lukasjenko alikuwa ametekeleza katika kufanikisha mpango wa kukomesha uasi, akisema kiongozi huyo amempa Wagner njia ya kuendelea kufanya kazi katika mamlaka ya kisheria.

Bosi huyo wa mamluki anaeleza kuwa kuandamana kwake kulisababisha vifo vya baadhi ya wanajeshi wa Russia wakati mamluki wa Wagner walipoangusha helikopta zilizokuwa zikiwashambulia.

"Hakuna hata mwanajeshi wangu mmoja aliyeuawa, tunasikitika kwamba tulilazimika kushambulia ndege, lakini walikuwa wakitupiga kwa mabomu na makombora," amesema. **BBC**

# ROBO FAINALI LIGI U-20 KUPIGWA LEO CHAMAZI

**Na Adam Fungamwango**

HATUA ya robo fainali ya Ligi ya Shirikisho la Mpira wa Miguu (TFF), kwa vijana chini ya miaka 20, inaanza leo katika Uwanja wa Azam Complex, baada ya kumalizika hatua za makundi.

Jumla ya timu nane zimefanikiwa kutinga hatua hiyo, huku timu za U-20 za Simba na Yanga zikitoa kapa.

**Robo fainali ya kwanza itakayochezwa saa nane mchana ni kati ya Geita Gold, kinara wa Kundi C dhidi ya Mbeya City ambayo ni mshindi wa pili wa Kundi A, na saa 10:15 jioni, kinara wa Kundi B, Dodoma Jiji FC itatoana jasho na Kagera Sugar iliyomaliza nafasi ya pili Kundi D.**

Saa 12:30 jioni, Mtibwa Sugar, aliyoongoza Kundi A itacheza dhidi ya Coastal Union, huku Azam FC kinara wa Kundi D, ikicheza dhidi ya Prisons ambayo ni mshindi wa pili wa Kundi C, muda wa saa 2:45 usiku.

Kwa mujibu wa TFF, nusu fainali itapigwa Juni 30 na fainali kuchezwa Julai 2, mwaka huu ambapo bingwa wa msimu wa 2022/23 atapatikana, wakati huu ambao Mtibwa Sugar ikiwa ndiyo timu inayolishikilia taji hilo mpaka sasa.

Yanga imeburuza mkia kwenye Kundi B, ikicheza mechi tatu haikushinda hata moja, sare moja ikipoteza michezo miwili, hivyo kumaliza mechi zake na pointi moja, huku Simba nayo ikiwa mkiani kwenye Kundi D, nayo kama wenzao Yanga, haijashinda mechi yoyote, sare moja na kupoteza mechi mbili, pointi moja peke yake ndiyo iliyovuna mwaka huu.

## Prisons yataja wakuwasajili, kambini mapema

**Na Saada Akida**

MWENYEKITI wa timu ya Tanzania Prisons, Enock Manguku, amesema baada ya wiki hii kukamilisha usajili wa nyota wanne wapya, Julai mwanzoni wataingia kambini kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya wa 2023/24 wa mashindano ya Ligi Kuu Tanzania Bara na Kombe la Shirikisho la Soka nchini maarufu FA Cup.

Aidha amesema kwenye usajili wao wataboresha nafasi nne ikiwamo kiungo wa juu, beki wa kati na washambuliaji wawili kulingana na mapendekezo ya ripoti waliyokabidhiwa na Kocha wao, Mohamed Abdallah 'Bares'.

Akizungumza na Nipashe jana, Manguku alisema suala la usajili tayari linaendelea kufanyiwa kazi kwa kuzungumza na baadhi ya wachezaji ambao Bares ameainisha katika ripoti yake kuwahitaji.

"Ni kweli kuna majina ya wachezaji tumepewa na kocha Bares, ila ni mapema kuwataja kwa sababu wengine wanawindwa na timu zingine, pia kuna zile nafasi nazo pia tunaangalia kina nani ambao watakuja kutusaidia na kwenda na falsafa za Tanzania Prisons," alisema mwenyekiti huyo.

Kuhusu kambi, alisema wataingia mapema sana kulingana na mipango ya kocha Bares kuwa na wachezaji pamoja kwa muda wa mwezi mmoja kabla ya kuanza rasmi kwa msimu wa 2023/24 wa Ligi Kuu.

Aliongeza kuwa wanatarajia kuweka kambi katika ardhi ya Tanzania na kuhusu ni mkoa gani, alisema wanatarajia kuangalia sehemu tulivu ambayo kocha na wachezaji watapata sehemu nzuri ya kujiandaa na msimu ujao wa ligi hiyo na mashindano mengine.

Msimu uliomalizika Prisons imemaliza katika nafasi ya nane ikivuna pointi 37 katika michezo 30 baada ya kushinda mechi 10, sare saba na kupoteza 13 huku ikiruhusu mabao 38 na kufunga 29 pekee.

## 'HOME SWEET HOME'...



Kipa wa Simba, Aishi Manula, akiwa nyumbani kwao baada ya msimu kumalizika huku akiendelea kuuguza majeraha kutokana na kufanyiwa upasuaji wa nyama za paja, katika picha hiyo aliyoipostí kwenye mtandao wake wa kijamii, ameandika: "Ni ardhi (Morogoro) yenye kuponya na kutia nguvu niwapo hapa najiona mwenye furaha na amani, sijawahi kuwa mnyonge ninapokuwa nyumbani kwa baba alipotuacha na mama."

## BMT yatoa rai Ligi ya Wavu

**Na Shufaa Lyimo**

BARAZA la Michezo la Taifa Tanzania (BMT), limeutaka uongozi wa Chama cha Mchezo wa Wavu Tanzania (Tava), kukaa na kuzungumza na viongozi wa vyama vya mikoa na wilaya kuhakikisha mchezo huo unachezwa kwa mtindo wa ligi ili kuibua vipaji vipya.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi usiku jijini Dar es Salaam wakati akifungua msimu wa pili wa Ligi ya Taifa ya mchezo huo inayoendelea kwenye Uwanja wa Gwambina, Dar es Salaam, Ofisa Michezo Mkuu wa baraza hilo, Alen Alex, alisema chama hicho kikifanya hivyo kitawapa fursa vijana shuleni nafasi ya kucheza na baadaye kupatikana wachezaji wengi chipukizi.

"Mchezo huu ukirudishwa shuleni ambapo ulipotea kwa kipindi kirefu, kwa kuchezwa Ligi ya Kata, Tarafa na Wilaya hapo watapatikana wachezaji chipukizi," alisema Alex.

Alisema Chama hicho kinapaswa kuzungumza na viongozi wa vyama vya mkoa pamoja na wilaya ili kuhakikisha mchezo huo unachezwa kwa mtindo wa ligi.

Alex alisema ligi hiyo itasaidia vipaji vya wachezaji wachanga na wakongwe kuonekana ikiwa ni pamoja na kupata kikosi cha timu za taifa zitakazokwenda nchini Cameroon (wanawake) na Misri (wanaume) kushiriki mashindano ya kimataifa ifikapo Agosti mwaka huu.

## Makocha Uhamiaji wafurahia kiwango

**Na Shufaa Lyimo**

BENCHI la ufundi la timu ya Netiboli ya Uhamiaji, limeeleza kufurahishwa na viwango vilivyoonyeshwa na wachezaji wao baada ya kuichapa Nyika Queens kwa mabao 67-52 katika mchezo waliocheza juzi jioni.

Timu hiyo imecheza jumla ya michezo tisa ikiwa ni mwendelezo wa michuano ya Klabu Bingwa Ligi Daraja la Kwanza, inayoendelea nje ya Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jana, Kocha Mkuu wa Uhamiaji, Winfrida Emanuel, alisema siri ya mafanikio yake ni mazoezi ikiwa ni pamoja na uangalizi mzuri wanaopewa na uongozi wa timu hiyo.

"Siri ya mafanikio yetu ni kutokana na mazoezi tunayoyafanya ikiwa ni pamoja na matunzo mazuri tunayopewa na uongozi wa uhamiaji kwa kutuwezesha kuja kushiriki mashindano haya, hivyo tunaahidi kutomuangusha," alisema Emanuel.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### RICE OFA MEZANI

KLABU ya West Ham imepokea ofa rasmi kutoka kwa Manchester City ili kumsajili kiungo wa kati wa England, Declan Rice mwenye umri wa miaka 24, katika mkataba wa thamani ya hadi pauni milioni 90. ***(The Athlete)***

### SPURS YAMTAKA MADDISON

KLABU ya Tottenham Hotspur inajiandaa kuwasilisha ofa ya pauni miloni 40 kwa mchezaji wa Leicester, James Maddison, 26, - lakini 'Foxes' wanataka pauni milioni 60 kwa nyota wao wa England. ***(Telegraph)***

### OSIMHEN LULU SOKONI

TAARIFA ya Napoli kukataa ofa ya euro milioni 100 kutoka Paris St-Germain kumnunua mshambuliaji wa Nigeria, Victor Osimhen, 24, inaweza kuwaibua Liverpool, Manchester United na Newcastle ambazo zipo tayari kutoa ofa nene. ***(Gazzetta dello Sport)***

### KANE NA BAYERN

KLABU ya Bayern Munich inaweza kuwa mbele ya foleni ya kumsajili mshambuliaji wa Tottenham Hotspur na England, Harry Kane, 29, ambaye anasemekana kutaka kuhamia Ujerumani. ***(Sky Sport Germany)***

### TINO ATAKIWA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United ipo kwenye mazungumzo ya juu na Southampton iliyoshuka daraja kuhusu mkataba unaowezekana wa pauni milioni 15 kwa beki wa pembeni wa England, Tino Livramento mwenye umri wa miaka 20. ***(Telegraph)***

### SANCHO, MAGUIRE KUUZWA

WACHEZAJI wa England, Jadon Sancho na Harry Maguire ni miongoni mwa nyota 13 ambao Manchester United wako tayari kuwauza msimu huu wa majira ya joto. ***(Mail)***

### RABIOT AOTA MBAWA UTD

MATAMANIO ya muda mrefu ya Manchester United ya kumsajili, Adrien Rabiot, 28, yanaweza kupata pigo tena kwa kiungo huyo wa kati wa Ufaransa kusaini mkataba mpya na miamba wa Serie A, Juventus. ***(Corriere dello Sport)***

### SALAH HAONDOKI LIVER

MOHAMED Salah, 31, hataondoka Liverpool hivi karibuni licha ya uvumi unaomhusisha fowadi huyo wa Misri kuhamia Saudi Arabia. ***(Mirror)***

### FOFANA AWINDWA ARSENAL

ARSENAL inamwona Youssouf Fofana, 24, kama mbadala wa kiungo wa kati wa West Ham, Declan Rice, lakini pia anawindwa na Newcastle United. ***(L'Equipe)***

### LOFTUS-CHEEK NA MILAN

AC Milan itamsajili aliyekuwa kiungo wa kati wa England, Ruben Loftus-Cheek, 27, kutoka Chelsea kwa euro milioni 15. ***(Calciomercato)***

### UNAI KUUNGANA NA TORRES

KOCHA wa Aston Villa, Unai Emery, anatamani kuungana tena na beki wa kati wa Villarreal, Pau Torres, 26, ambaye atagharimu chini ya pauni milioni 51. ***(Times)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MADRID BADO YAKOMAA KUMNG'OA MBAPPÉ PSG

**●●● Atengewa jezi ya Benzema ili kwenda kushirikiana na Vinicius na Rodrygo...**

**MADRID,** Hispania

REAL Madrid bado inaangalia kwa makini uwezekano wa kumsajili Kylian Mbappé, lakini klabu hiyo pia ina matumaini kwamba makubaliano yanaweza kufikiwa kumpata mshambuliaji huyo wa Paris Saint-Germain msimu huu wa majira ya joto.

**Kuna kusitasita kuzungumza kwa uwazi kuhusu ujio wa Mbappé pale Bernabeu baada ya majira ya joto yaliyopita mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ufaransa kusaini mkataba mpya na PSG wakati alikuwa anakaribia kuhamia Madrid.**

Msimamo wa klabu hiyo kwa umma ni kwamba shughuli yao ya soko la uhamisho imekamilika baada ya kusajiliwa kwa Jude Bellingham, Joselu, Fran García na Brahim Díaz.

Hata hivyo, ukweli ni kwamba klabu hiyo imeiacha wazi jezi namba tisa iliyokuwa ikivaliwa na Karim Benzema ambaye amekwenda kujiunga na Al Ittihad kwa sababu kuna matumaini pia kwamba Mbappé anaweza kupatikana.

Vyanzo vimeiambia ESPN kuwa hakuna maendeleo makubwa tangu Mbappé atangaze mnamo Juni 12 kuwa alikuwa ameiambia PSG kwamba hatakuwa na chaguo la kuongeza mkataba wake zaidi ya mwaka 2024.

Hadharani, Mbappé ameendelea kusisitiza kwamba anataka kuendelea PSG kwa msimu mmoja zaidi, lakini vyanzo vingi vimeiambia ESPN kwamba mchezaji huyo anataka kusaini Madrid msimu huu wa majira ya joto.

PSG ingependa kuzuia kumpoteza kwa uhamisho wa bure mwaka ujao na kwamba Madrid wako tayari kufanya juhudi kubwa kuona Mbappé akiongoza mashambulizi yao pamoja na Vinícius Júnior na Rodrygo.

Madrid wako macho na wana matumaini kwamba harakati zao za muda mrefu zinaweza kuzaa matunda msimu huu wa majira ya joto, kwa kujua kwamba PSG ingependa kupunguza matumizi yao kulingana na vikwazo vya usawa wa kifedha.

Chanzo kiliiambia ESPN kwamba sakata la uhamisho wa majira ya joto usiotarajiwa unaweza kufanyika.

Kocha wa Madrid, Carlo Ancelotti, alitaka kuona safu yake ya mbele ikiimarika msimu uliopita wa joto kwa kuungana na Benzema, na hitaji hilo ni kubwa zaidi kwa kuwa mshindi huyo wa Ballon d'Or ameondoka kwenda Saudi Arabia.

Kocha huyo raia wa Italia anamtazama mchezaji wa kimataifa wa Hispania, Joselu aliyesajiliwa kwa mkopo kutoka Espanyol -- kama mbadala badala ya kuwa mwanzilishi na ukweli ni kwamba alipewa jezi namba 14, badala ya tisa ya Benzema.

Madrid walishindwa kutetea mataji yao ya LaLiga na Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita - wakishinda Copa del Rey, UEFA Super Cup na Kombe la Klabu Bingwa Dunia.

# MAN CITY YATUMA OFA YAO KWA RICE



**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester City imewasilisha ombi lao la kwanza rasmi la kumnunua nahodha wa West Ham United, Declan Rice, kwa mujibu wa 90minutes.

Mabingwa hao wa Ligi Kuu England wamekuwa wakijiandaa kuchuana na Arsenal kwa Rice, ambaye hivi majuzi alifuata nyayo za nguli wa West Ham, Bobby Moore na Billy Bonds kumaliza miaka 43 ya klabu hiyo ya kusubiri kombe.

Arsenal tayari wamekataliwa ofa mbili na West Ham - ofa ya mwisho ya pauni milioni 75 kama fedha ya uhakika pamoja na nyongeza ya pauni milioni 15 - na kuna matarajio kwamba ofa ya tatu itawasilishwa hivi karibuni baada ya mazungumzo ya muda mrefu kati ya klabu hizo mbili.

Lakini City sasa wanataka kuipiku Arsenal kwa kutoa ofa yao rasmi yenye thamani ya pauni milioni 80 katika fedha ya uhakika pamoja na pauni milioni 10 za nyongeza.

Mmiliki wa West Ham, David Sullivan, amekiri hadharani kwamba Rice huenda akaondoka katika klabu hiyo msimu huu wa majira ya joto - mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, amezungumza kuhusu nia yake ya kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Dau la City ni pungufu ya kiasi hicho, lakini inaaminika kuwapa West Ham kiasi kikubwa cha fedha mbeleni, tofauti na ofa ya Arsenal ambayo ilipangwa kutoa malipo kwa miaka kadhaa.

Rice amebakiza miaka miwili kwenye mkataba wake kwa sababu West Ham wana chaguo la kuongeza mkataba wake zaidi ya msimu wa majira ya joto wa 2024, na amekuwa mmoja wa wachezaji wanaohitajika sana katika soka la Ulaya kwa sasa.

Manchester United, Bayern Munich na Chelsea ni klabu nyingine tatu zinazowania saini ya mchezaji huyo.

# Diaz abadilishiwa jezi Liver




**LIVERPOOL,** England

LIVERPOOL imethibitisha kuwa Luis Diaz hatavaa tena jezi namba 23 aliyokuwa anavaa tangu alipojiunga na klabu hiyo akitokea FC Porto Januari mwaka jana.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, aliona kampeni yake ya kwanza kamili Anfield ikivurugwa na majeraha, akicheza mechi 21 pekee katika mashindano yote.

Diaz bado alisajili mabao matano kwa 'Wekundu' hao wakati huo na kufikisha idadi yake ya mabao hadi 11 katika mechi 47 alizocheza nchini England.

Katika majira haya ya joto ya mabadiliko pale Liverpool, klabu tayari imethibitisha kuwa mchezaji mpya Alexis Mac Allister atavaa jezi namba 10, ambayo ilikuwa ikivaliwa na Sadio Mane na Philippe Coutinho, lakini Diaz pia atapewa namba mpya msimu wa 2023/24.

Kuondoka kwa James Milner katika klabu hiyo kumefungua fursa kwa Diaz kutwaa jezi namba saba iliyojaa heshima na historia.

Kenny Dalglish, Luis Suarez na Peter Beardsley ni wachezaji watatu wanaoheshimika zaidi kuwahi kuvaa namba hiyo, huku Steve McManaman, John Aldridge na Ian Callaghan pia waliwahi kuvaa jezi hiyo.

Jezi hiyo ilikuwa inavaliwa na Milner kwa miaka nane.

Milner aliichezea Liverpool mara 332 katika mashindano yote, akifunga mabao 26, na alikuwa sehemu muhimu ya kikosi kilichomaliza kipindi cha miaka 30 cha kusubiri taji la Ligi Kuu England mwaka 2020.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 37, pia alishinda Ligi ya Mabingwa Ulaya, Kombe la Klabu Bingwa Dunia, Super Cup, FA, Carabao na Ngao ya Jamii wakati alipokuwa Liverpool, kabla ya kuhamia Brighton.

# AC Milan yajitosa kwa Loftus-Cheek

**MILAN,** Italia

AC Milan wamerejea tena kutaka kumnunua kiungo wa kati wa Chelsea na England, Ruben Loftus-Cheek, vyanzo vimethibitisha kwa 90minutes.

Miamba hiyo ya Ligi Kuu Italia, Serie A, ambao wameidhinisha kuondoka kwa Sandro Tonali kwenda Newcastle United, wako sokoni kwa ajili ya kuimarisha safu ya kati huku wakipania kujiimarisha baada ya kutinga nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita.

Kikosi hicho cha kocha Stefano Pioli kimekuwa kikijaribu kuweka makubaliano ya kumnunua David Frattesi wa Sassuolo, lakini wanakabiliwa na ushindani mkubwa kutoka kwa wapinzani wao wa jiji moja Inter Milan, ambao wanatafuta kuchukua nafasi ya Marcelo Brozovic anayelengwa na Barcelona na Saudi Arabia.

Milan walikuwa wameanza mazungumzo na Chelsea Mei mwaka huu kuhusu mpango wa kumnunua Loftus-Cheek, lakini 'Rossoneri' hao wakamfukuza Mkurugenzi wa Ufundi, Paolo Maldini na Mkurugenzi wa Michezo, Ricky Massara, ambao ndio walikuwa wameanza mchakato wa kumtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27.

Mazungumzo yameanza tena kati ya Milan na Chelsea, na pande hizo mbili zilizungumza mwishoni mwa juma ili kupanga jinsi ya kuendelea - walijadili pia upatikanaji wa Conor Gallagher, Christian Pulisic na Pierre-Emerick Aubameyang.

Chelsea imekuwa ikitafuta kupokea ada ya takriban pauni milioni 20 kwa Loftus-Cheek, lakini inaaminika kuwa Milan wanatarajia kufikia makubaliano yenye thamani isiyozidi pauni milioni 17.

Loftus-Cheek amebakiza miezi 12 tu kwenye mkataba wake msimu huu wa majira ya joto na tayari ameambiwa na Chelsea kwamba anaweza kuhama.

Iwapo Loftus-Cheek ataondoka Chelsea msimu huu wa majira ya joto, ataungana na wachezaji wengi wanaoelekea kwenye mlango wa kutokea huku klabu hiyo ikijiandaa kuingia katika zama mpya chini ya kocha Mauricio Pochettino.

N'Golo Kante na Kalidou Koulibaly tayari wameondoka na kujiunga na Al Ittihad na Al Hilal, huku Edouard Mendy na Hakim Ziyech nao wakiwa njiani kuelekea Saudi Arabia kujiunga na Al Ahli na Al Nassr.



## Simba yaanika hatima mkataba na Sawadogo

INATOKA UKURASA 24

anaidai klabu hiyo, Ahmed alisema wamemalizana na nyota huyo na hawana muda wa kubishana na mchezaji ambaye ameshindwa kuonyesha kiwango chake ndani ya Simba na hata alipopelekwa kwa mkopo Ihefu FC.

"Kama kweli Okwa au kuna mchezaji ambaye tumemuacha anaidai Simba basi niwaombe waende kushtaki katika mamlaka husika, ninaimani kuwa hakuna mchezaji anadai kwa wale tulio-waacha," alisema Ahmed.

Alisema baada ya wiki hii kukamilisha zoezi la kuwapa asante wachezaji ambao hawataendelea nao kwa msimu mpya wa 2023/24, watatangaza rasmi benchi la ufundi kwa wale watakaoziba nafasi ya walioondoka halafu usajili wa wachezaji wapya na baadaye wataeleza ni wapi wataenda kuweka kambi.

Taarifa zilizoifikia gazeti hili ni kwamba hadi sasa kuna nchi tatu ambazo ni Canada, Uturuki na Afrika Kusini, ambapo Simba iko kwenye mchakato wa wapi waende kwa ajili ya kujiandaa na msimu mpya.

# YANGA: HATUJAFUNGIWA FIFA, MAJEMBE 'MAKALI' YANAKUJA

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imekanusha taarifa zilizoanza kusambaa juzi jioni kwenye mitandao ya kijamii kuwa imefungiwa kusajili kutokana na kushindwa kumlipa kocha wake wa zamani, Luc Eymael, ikizielezea kuwa ni propaganda za watu walioshindwa huku ikiahidi kushusha majembe ya uhakika hivi karibuni.

**Ofisa Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ali Kamwe, amesema walikiri kupokea barua ya kumlipa kocha huyo tangu Machi, mwaka huu na waliitolea ufafanuzi, huku kocha mwenyewe akithibitisha hilo, lakini anashangaa zilipotokea taarifa hizo juzi.**



"Hizi ni taarifa za uongo, hatujafungiwa na FIFA, hizi ni propaganda za watu walioshindwa, nawataka wanachama na mashabiki wa Yanga kuzipuuza, wasiyumbishwe na maneno yasiyo ya kweli, taarifa kamili za klabu zitatolewa na vyombo vya klabu yenyewe," alisema Kamwe.

Katika kusisitiza kuwa hazikuwa taarifa za ukweli, alisema hazipo kwenye kurasa za Shirikisho la Kimataifa la Soka (Fifa), hususan kwenye kitengo kinachoshughulikia suala hilo, ambapo kama zingekuwa sahihi zilitakiwa zianzie huko na kusambaa, siyo zionekane tu kwenye mitandao ya kijamii.

Hata hivyo, alikiri kuwa wanadaiwa na kocha huyo na walishaliweka suala hilo bayana, lakini kuhusu kumlipa, alisema si jambo la busara kuliweka hadharani.

"Tulikiri kupokea barua ya Fifa na makubaliano ilikuwa ni kumlipa kwa awamu, tukasema tunalifanyia kazi, ila siwezi kuja hadharani kueleza nini kinaendelea kwenye makubaliano haya ambayo yanafanyiwa kazi, haya ni mambo ya taasisi kwenda kwa mhusika mwenyewe, tunawaomba tu wanachama na mashabiki wa Yanga kuwa watulivu.

"Tuko kwenye maandalizi ya msimu unaokuja, sasa hivi viongozi wanajiandaa kutoa jezi za msimu unaokuja, kutambulisha wachezaji wapya tunaowasajili kwa sababu hatujafungiwa na kuandaa 'pre season' kama unavyofahamu tutacheza mechi za Ngao ya Jamii mapema sana mwezi wa nane na safari hii zitachezwa kama ligi pamoja na Tamasha la Wiki ya Mwananchi," Kamwe alizidi kufafanua.

Kocha huyo raia wa Ubelgiji aliifundisha Yanga kuanzia Januari 2020 hadi Julai mwaka huo alipotimuliwa kwa madai ya kutoa maneno ya kibaguzi.

Tangu wakati huo kocha huyo amenukuliwa akidai anaidai klabu hiyo, ambapo Machi mwaka huu ziliibuka taarifa kama hizi za Yanga kufungiwa madirisha matatu ya usajili, lakini mwenye Eymael aliibuka na kukiri anadai na kukanusha kuwa klabu hiyo imefungiwa.

"Nadhani walioandika taarifa hiyo wameripoti kinyume, tumejulishwa kwamba Yanga wanatakiwa kunilipa stahiki zangu ndani ya siku 45 na iwapo wakishindwa kufanya hivyo kuna adhabu kubwa, ila hawajafungiwa kusajili, wamejulishwa uamuzi wa kutakiwa kunilipa fedha zangu," alisema Eymael Machi mwaka huu.




Mashabiki wa soka Kigoma wakiwa wamefurika kwenye Uwanja wa Central mkoani humo, wakiilaki timu ya soka ya Mashujaa FC ikiingia ikitokea jijini Mbeya ilipofanikiwa kutinga Ligi Kuu, kwa kupata ushindi wa jumla wa mabao 4-1. Bao 1-0 ugenini na nyumbani 3-1. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *Mashujaa yapokewa kishujaa kwao Kigoma*

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha timu ya Mashujaa FC kimewasili mjini Kigoma juzi kikitokea jijini Mbeya na kupokewa kishujaa na mamia ya maelfu ya mashabiki wa timu hiyo na baadhi ya viongozi wa vyama mbalimbali na serikali.

Jumamosi iliyopita ikiwa Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya, Mashujaa FC iliweka historia ya kupanda Ligi Kuu Tanzania Bara ilipoifunga Mbeya City bao 1-0, ikimaliza ukame wa miaka 20 kwa mkoa wa Kigoma kutokuwa na timu ya mpira wa miguu kwa ngazi hiyo.

Mashujaa ilifanikiwa kutinga Ligi Kuu kwa jumla ya mabao 4-1, baada ya mechi ya kwanza kushinda 3-1 katika Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma.

Ilikuwa hoi hoi nderemo ya vifijo, pale msafara wa magari ulipoingia mjini Kigoma, ukitokea Mpanda mkoani Katavi, ulipokuwa umetia nanga kwa muda baada ya kuwasili kutoka jijiji Mbeya.

Msafara huo ambao ulipita barabara kadhaa mjini Kigoma, ulitimisha safari yake kwenye Uwanja wa Central mkoani humo na kupokewa na viongozi mbalimbali.

Mkuu wa mkoa huyo, Thobias Andengenye, ambaye alikuwa kwenye msafara uliotoka Mbeya, aliwataka wananchi wa mkoa huo na mashabiki, kuitunza na kuisapoti timu hiyo kama mboni ya jicho na alitaka wailinde ili isishuke daraja kwani kuipandisha timu Ligi Kuu ni kazi ngumu.

"Timu hii itunzwe kama mboni na kufanyiwa kila aina ya hisani, tusikubali kurudi tena nyuma kama ilivyokuwa miaka 20 iliyopita, tunafahamu ugumu wa kuvuka mstari kutoka Ligi ya Championship na kuingia Ligi Kuu Tanzania Bara," alisema mkuu huyo wa mkoa.

Naye Mjumbe wa Bodi ya klabu hiyo, aliyejitambulisha kama Meja Tika, alisema hawaendi kinyonge kwenye Ligi Kuu, badala yake watajiandaa kikamilifu kwa usajili kabambe.

"Hatuendi kinyonge tunafanya usajili mzuri, tuko makini, tunataka Jeshi la Wananchi (JWTZ), liwe na timu imara kuliko timu zote za majeshi zilizowahi kucheza Ligi Kuu," alisema meja huyo.

Timu ya mwisho kucheza Ligi Kuu Kigoma, ni Reli FC miaka 20 iliyopita, ambayo ilipanda baada ya kushuka kwa timu ya Mbanga FC.

Kabla ya hapo, Kigoma ilikuwa pia na timu ya RTC Kigoma iliyofanya makubwa wakati huo ligi ikiitwa Ligi Daraja la Kwanza Tanzania Bara.

Michezo
Jumatano Juni 28, 2023
Nipashe



Madrid yamkomalia Mbappé UKURASA 21

# Simba yaanika hatima mkataba na Sawadogo

**●●● Pia yamshangaa Okwa, yamtaka kama ana hoja aende Fifa, huku...**



Ismael Sawadogo

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Simba umesema wanatumia utaratibu mzuri kulingana na vipengele vya mikataba yao na wachezaji inapofika hatua ya kuachana na mchezaji ambaye bado mkataba wake na klabu upo hai, jambo ambalo pia wanalitekeleza kwa kiungo mkabaji Ismael Sawadogo kabla ya kumpa 'thank you'.

**Kauli hiyo imetolewa na Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally, baada ya madai kuwa klabu hiyo inashindwa kuachana na Sawadogo kutokana na kuitaka kumlipa Sh. milioni 700 ili kuvunja mkataba wake.**

Akizungumza na Nipashe jana, Ahmed alisema mchezaji anaposaini mkataba na Simba kuna makubaliano yanakuwapo mwanzoni ya jinsi ambavyo akishindwa kuendelea kutumikia klabu hiyo au viongozi wakihitaji kuvunja mkataba wanachotakiwa kukifanya kwanza.



Alisema Sawadogo ana mkataba wa mwaka mmoja na wako kwenye mazungumzo ya kutoendelea naye kwa msimu ujao na baada ya maafikiano ya pande zote mbili wataweka wazi kuachana naye rasmi.

Ahmed alisema Simba inaendeshwa kisasa katika mazungumzo hayo na si suala la fedha kwa sababu kabla ya kusaini mkataba kuna kipengele ambacho kiko wazi mchezaji au klabu atakapovunja mkataba na anapouzwa nini kifanyike kabla.

"Hayo masuala la Sh. milioni 700 sijui yametoka wapi kwa sababu kila kitu kipo wazi, ni kweli Sawadogo hatutaendelea naye kwa msimu ujao na tuko kwenye mazungumzo ya kuvunja mkataba wake," alisema Ahmed.

Aliongeza kwa suala la fedha ya kumlipa mchezaji halijadiliwi bali linakuwapo kwenye mkataba ambao wanaingia naye anaposaini kuitumikia klabu hiyo na hadi sasa hakuna mchezaji ambaye ameachana nao anayedai haki zake.

Kuhusu kiungo Mnigeria Nelson Okwa, ambaye amekuwa akitoa maneno mengi baada ya kuachwa na Simba, huku akisema

INAENDELEA UKURASA 23

## Man City yatuma ofa yao kwa Rice

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester City imewasilisha ombi lao la kwanza rasmi la kumnunua nahodha wa West Ham United, Declan Rice, kwa mujibu wa...



HABARI UKURASA 22



Eng. Hersi Said

## Yanga yaruka kufungiwa Fifa kusajili

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imekanusha taarifa zilizoanza kusambaa juzi jioni kwenye mitandao ya kijamii kuwa imefungiwa kusajili kutokana na kushindwa...

HABARI UKURASA 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >